# KUCHUNGUZA DHIMA YA NYIMBO KWA WAFIWA KATIKA JAMII YA WANYAKYUSA WILAYA YA RUNGWE, MKOA WA MBEYA

**TIMOTHY AMANYISYE KIBUNGU**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA KUKAMILISHA MASHARTI YA**

**KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA**

**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyesaini hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma na anapendekeza tasnifu hii inayoitwa: "**Kuchunguza Dhima ya Nyimbo kwa Wafiwa Katika Jamii ya Wanyakyusa Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya"**, na kupendekeza, ikubaliwe ikubaliwe kwa minajili ya kutahiniwa ili kutnukiwa shahada ya uzamili (MA: Kiswahili Fasihi) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……………………………………………….

**Prof. Tigiti S.Y.M. Sengo**

**(Msimamizi)**

…………………………….……….

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe amakazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeleo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taalumaza Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TAMKO

Mimi, **Kibungu Timothy Amanyisye**, ni nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya Digrii yoyote.

…………………………………………..

Saini

……………………………………………

Tarehe

# TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu kwa kunisomesha, hadi leo nimefikia hatua hii ya uzamili.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaaliya afya njema kipindi chote cha masomo yangu, hekima, na busara na maarifa katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Ahimidiwe Mola Mwenye enzi yote.

Tunapenda kuwashukuru Maprofesa na wahadhiri wetu wote, kwa kazi ya kuelimisha watu; Prof. Emanuel Mbogo, Dkt. A. Kishe, Dkt. O. Mohamed na Bw. E. Msangi, kwa kutiliya mbolea na dawa katika ilimu na ujuzi wa somo la Fasihi ya Kiswahili na Utafiti.Hata kuwa kichocheo kwetu kwenda maskani kufanya utafiti. Mola, Mungu, Mwenyezi awajalie moyo mwema huo wa kitume na azidi.

Shukurani za pekee ni kwa wazazi wangu kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha. Kwa uvumilivu wao, kwa kujitoa kwa hali na mali, kwa hisani ya baraka ya maombi yao kuweza kuhitimu masomo yangu ya shahada ya uzamili. MUNGU awajaliye neema ya uzima na baraka tele pia naomba MUNGU awabariki.

Ninapenda kutoa shukuranizangu za dhati kwa Msimamizi wangu Prof. Tigiti S.Y.M. Sengo kwa kunilea kitaaluma na kunikuza katika misingi ya nadharia na vitendo katika fasihi ya Kiswahili.  Ninamtakiya neema ya uzima na baraka kwa MOLA Mtukuka, maisha marefu ili azidi kuwa hazina ya taaluma kwa wenye kiu ya kuisaka. Tutakuwa wachache wa fadhila, tusipotoa shukurani kwa wanaidara wote, wa idara ya lugha na fasihi kwa kutupatiya ushauri, maoni na miongozo katika kutufanikisha kumaliza kozi kwa mafanikio makubwa.

Ninawashukuru wanataalimu watangulizi, kina Mbwana, Mgogo, Mwabuka walionishauri na kutuongoza kwenda Maskanini, wakati mwingi, kunisaidia ukalimani. Pia ninamshukuru sana Bi Ghati mwanataalimu, mshauri na mtia moyo, Mungu Ambariki.

Mwisho, ninaishukuru sana familia ya mdogo wangu Isihaka Mafwenga, ilivyonihudumia na kunivumilia wakati wote, Mungu Awabariki mno. Nawashukuru watafitiwa wote walionisaidia kufikia mafanikio ya utafiti huu na wale wote walionisaidia kukamilisha tasnifu hii.

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti wetu lilikuwa kuchunguza dhima ya nyimbo kwa wafiwa katika jamii ya Wanyakyusa wa Kata ya Lufingo, kijiji cha Ighembe (Kalalo), Itete, Kagwina, na Simike, wilaya ya Rungwe, mkoa wa Mbeya. Malengo mahususi yalikuwa ni kubainisha dhima za nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa, Kuchambua dhamira katika nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa na kuelezea uhalisia wa nyimbo hizo kwa jamii ya leo. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na ushiriki na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa nyimbo hizo zina dhima ya kuelimisha, kukosoa jamii, kuliwaza, kuhimiza watu kufanya mambo mema na kutunza mila na dasturi za jamii. Kwa upande wa dhamira zimekuwepo dhamira za malezi mema, kifo, kumuombea marehemu, kutoogapa kifo na kumuogopa Mwenyezi Mungu. Kwa jumla dhamira hizi zina uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii kwani kila mtu ataonja umauti na hivyo ni vizuri kufanya matendo mazuri ili kuweza kuishi vizuri katika kipindi chote cha uhai wa mtu hapa duniani.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHI** .................... **ii**

**HAKIMILIKI** .................... **iii**

**TAMKO** .................... **iv**

**TABARUKU** .................... **v**

**SHUKRANI** .................... **vi**

**IKISIRI** .................... **viii**

**ISTILAHI ZILIZOTUMIKA** .................... **xiii**

**SURA YA KWANZA** .................... **1**

**1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO** .................... **1**

1.1 Utangulizi .................... 1

1.2 Mapisi na Asiliya ya Wanyakyusa .................... 1

1.2.1 Jiografia Yao .................... 4

1.2.2 Hali ya Hewa .................... 5

1.2.3 Utamaduni .................... 5

1.2.4 Mila .................... 5

1.2.5 Dasturi .................... 6

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti .................... 6

1.3.1 Dhana ya Mfiwa / Wafiwa .................... 6

1.3.1.1 Historia Mfiwa .................... 6

1.3.2 Dhanna ya Nyimbo .................... 7

1.3.3 Dhanna ya Dhima .................... 7

1.3.4 Chimbuko la Nyimbo kwa Wafiwa .................... 7

1.4 Tatizo la Utafiti .................... 10

1.5 Lengo Kuu ........ 12
1.6 Madhumuni Mahususi ........ 12
1.7 Maswali ya Utafiti ........ 12
1.8 Umuhimu wa Utafiti ........ 12
1.9 Mipaka ya Utafiti ........ 13
1.10 Mpangilio wa Tasnifu ........ 13
**SURA YA PILI ........ 15**
**2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........ 15**
2.1 Utangulizi ........ 15
2.2 Dhima za Nyimbo katika Jamii ........ 15
2.3 Fani katika Nyimbo ........ 17
2.4 Mkabala wa Kinadharia ........ 19
2.4.1 Nadharia ya Saikiolojia Changanuzi ........ 20
2.5 Hitimisho ........ 22
**SURA YA TATU ........ 23**
**3.0 MBINU ZA UTAFITI ........ 23**
3.1 Utangulizi ........ 23
3.2 Eneo la Utafiti ........ 23
3.3 Usanifu wa Utafiti ........ 23
3.4 Aina za Data Zilizokusanywa ........ 24
3.4.1 Data za Msingi ........ 24
3.4.2 Data za Upili ........ 24
3.5 Uteuzi wa Watafitiwa ........ 25

3.6 Mbinu za Kukusanya Data ....... 25

3.6.1 Mbinu ya Usaili ....... 25

3.7 Mbinu ya Ushiriki ....... 26

3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data ....... 27

3.9 Hitimishi ....... 27

**SURA YA NNE ....... 28**

**4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ....... 28**

4.1 Utangulizi ....... 28

4.2 Dhima ya Nyimbo za Msiba ....... 28

4.3 Mjadala wa Data za Utafiti ....... 52

4.3.1 Kufariji Wafiwa ....... 52

4.3.2 Kurithisha Utamaduni, Mila na Dasturi ....... 52

4.3.3 Kuhimiza Umoja ....... 52

4.3.4 Kuonya Jamii ....... 53

4.3.5 Kusifia Uwajibikaji ....... 53

4.4 Fani katika Nyimbo kwa Wafiwa ....... 53

4.5 Hitimishi ....... 53

**SURA YA TANO ....... 55**

**5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO ....... 55**

5.1 Utangulizi ....... 55

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ....... 55

5.3 Matokeo ya Utafiti ....... 56

5.4 Mapendekezo ....... 56

5.5 Hitimishi .......... 58

**MAREJELEO .......... 60**

**VIAMBATANISHO .......... 64**

## ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

| | |
|---|---|
| Malafyale | Chifu, ntemi, mfalme. |
| Nselya | Ng'ambo ya mto |
| Kusoka | Kuonya, kukemea |
| Kinyonyi | Chombo cha kubebea taarifa.flashi au CD |

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO

## 1.1 Utangulizi

Sehemu hii inaelezeya mapisi na asiliya ya Wanyakyusa, usuli wa tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahususi ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka yautafiti na mpangilio wa tasnifu.

## 1.2 Mapisi na Asiliya ya Wanyakyusa

Wanyakyusa ni neno lililojengwa kwa jina (nomino) kyusa, sifa ukeni. Pia neno hilo limesimamia umoja na wingi Wanyakyusa. Kyusa ni jina la mke mdogo wa mfalme (malafyale) aliyekuwa na wake wengi. Neno wanya lina maana ya watoto wa fulani. Jina hilo la Wanyakyusa kutokana na masimulizi ya mapokeo kutoka kwa wazee yasemekana, kuwa mfalme alipokuwa amekaribia kufa alihitaji mrithi, hivyo palitokea mzee kikongwe mmoja, kuhani, nabii ambaye alipita kila nyumba ya wakezeili kumtia mafuta atakayekuwa mfalme (malafyale). Katika nyumba zingine hawakumkarimu wala hakuona mtoto mwenye khekima ya kutawala na kuongoza. Yasemekana kuwa nabii au kuhani huyo alikuwa kama mzee mchafu asiyetamanika kabisa. Mwisho alikwenda nyumba ya mke wa mwisho wa malafyale aliyeitwa kwa jina Kyusa kwa upande wa baba yake. Alipofika, alikaribishwa kwaukarimu na kwa moyo wa kuchangamuka. Alimpatia maji ya kuoga, alimwandalia chakula kinono, na kisha alimuuliza malafyale kama ana watoto wa kiume katika nyumba ile. Walikuwepo vijana wakubwa lakini hawakupata kibali mbele ya mgeni. Kisha akauliza kama hakuna kijana mwingine?

Alimjibu yupo lakini hayupo karibu, ila yuko malishoni (ndukubo). Mzee mgeni alimwomba mfalme atume wajumbe wake wamfuate malishoni. Alipofika palifanyika sikukuu ya kumtiya mafuta, kumtawaza awe malafyale mtoto wa mwanamke aliyeitwa kyusa. Katika harakati ya kumpata mtawala kutoka kwenye nyumba ndogo ya kyusa ndipo jamii zote zilipoanza kuitwa kwa sifa ya malikiya kwa jamii ya kyusa (Mnyakyusa-umoja, wingi-Wanyakyusa). Mabadiliko hayo yalifanyika kipindi cha utawala wa Waingereza walipoanza kutawala Tanganyika.

Hapo nyuma kabla ya Wajerumani, Wanyakyusa walijulikana kwa jina la wasokile. Hii ni kutoka lugha ya nzuri ya kuamkiana. Ambayo walisalimiana mwemusokile, musokile na kujibu tusokile / nsokile. Kwa maana kusema habari ya kuamka na kujibu nimeamka salama/ tumeamka salama. Kubadilika kwa lugha kumetokana na nadhariya ya mabadiliko na mwingiliano wa koo mbalimbali.

Aidha naweza kusema kuwa Wasokile ama Wanyakyusa wametokana na jamii ndogo ndogo nyingi. Lakini jamii kubwa niwanyakyusa wabungu, wanyakyusa Wanselya na Wanyakyusa Wangonde. Wanyakyusa wabungu wana majilio yao, inaaminika kuwa ni watu waliotoka magharibi na maongilio yao ni Usangu ambao walipitia milima ya Ukinga-Umbwila, na kuingia Rungwe. Hawa watu katika masimulio yao wanasema, waliwakuta watu waliokuwa wanakula matunda na mizizi, wanyama na ndege. Wanyakyusa wabungu walikuwa watu wenye nguvu na hodari kuwinda,  kulima na kufuga ng’ombe. Hivyo wenyeji waliwategemea sana kwa chakula na kwa usalama wao. Masimulizi kutoka mzee Mwakisumusya Rungwe –IBUNGU (Kalalo 12/02/2016).

Wanyakyusa Wanselya yasemekana walitokea mashariki- kupitia Iringa-Mahenge. Ambao walikuta wanyakyusa Wabungu wanaishi Rungwe kwa amani kabsa. Wanyakyusa Wanselya wakiongozwa na Mwakapalila walipofika mwambao mwa milima Rungwe-Kabale walidhani wanyakyusa Wabungu wangewapiga kwa vile walivyokuwa wamesifika sana kwa amani na maendeleo. Kuhakikisha Mwakapala wanyakyusa Wabungu kwenye sherehe walikubali. Hivyo, walishirikiana katika masuala ya jamii kama vile; ndoa, vifo na mambo mengine.

Wanyakyusa jamii ya Wanyangomole yasemekana ilitokea Malawi, yumkini walitoka Afrika ya kusini kwa Wazulu, majilio yao yalitokana na vita na njaa kwa sababu ya ukame wa muda mrefu, ambao ulisababisha vifo kwa watu wengi na mifugo pia. Hivyo walivuka ziwa nyasa kupitia mto songwe. Sauti ya Vijana wa Busokela, Rungwe mashariki wanaungana na madhariaya ya historiya. Wanamini kuwa asiliya yao ni Morogoro, ambao walikimbia vita, na hali mbaya ya hewa. Wanaosema kuwa mwindaji wa Kiruguru alifika eneo la Kabale lililopo Suma-Rungwe na kukutana na Mzulu toka Afrika kusini ambaye naye alikuwa mwindaji aliyekuwa na binti yake.

Kati ya wawindaji hao wawili Mzulu alikuwa hafanikiwi kwenye mawindo yake, bali yule Mluguru alikuwa anafanikiwa kila mara. Mwisho alitokea kuwa mfadhiriwa mzulu na matokeo yake, alimpa binti yake kuwa mke wake (mluguru). Wanasema kwa sababu ya harufu ya nyama waliyokuwa wameikausha kwa muda mrefu kwa moto ilikuwa inatoa harufu. Eneo hilo lilijawa na harufu kila siku. Mzulu alisema, “pale panatoa kyusi kila siku.” Kwa maana ya moshi kwa lafudhi

ya lugha ya Kizulu. Kutokana na mazoea ya kutamka neno la “kyusi” likageuka na kuwa Kyusa. Hivyo ikatokea kumwita mluguru “wanyakyusa”. Hivyo watoto waliokuwa wanazaliwa na wageni wengine wakaitwa wanyakyusa. Asili na chimbuko la wanyakyusa ni Kabale na kabila mbili la Mluguru na Mzulu na utawa ulianzia hapo.

Muunganiko wa watu kutoka pande tatu mashariki –Nselya, magharibi (Abangumba), Wabungu (Abamwamba) na Wangonde (Bantebela) ndiyo asiliya, chimbuko ya wanyakyusa Kabale mwambaoni mwa mlima Rungwe. Ndiyo asiliya ya makabila mengi; Wandali, Wamalila, Wasafwa, Wayao, Wakagulu, Wafipa, Wabungu na wengine waishio kando kando ya milima na wenye utamaduni, mila na dasturi moja.

### 1.2.1 Jiografia Yao

Wanyakyusa ni miongoni mwa makabila makubwa yaishiyo nchini Tanzania. Wanyakyusa wanapatikana mkoa wa Mbeya nyanda za juu kusini, wilaya ya Rungwe. Ingawa watu hao wameenea nchini na nchi nyingine. Hapo mwanzo wilaya hiyo ilijumuisha wilaya ya Kyela, na Ileje. Wenyeji wa wilaya zote wanaongeya lugha moja, ina maana wana utamaduni, mila na dasturi unaofanana kwa sababu asiliya na mapisi ya aina moja.

Wilaya ya Rungwe kwa upande mashariki inapakana na wilaya ya Makete, mkoa wa Njombe, magharibi inapakana na wilaya ya Ileje, na kaskazini inapakana wilaya ya Mbeya vijijini,na kusini wilaya ya Kyela.Ni wilaya iliyozungukwa na

safu za milima pande zote.Watu wanaishi kwenye nyanda milima.Ndani yake kuna chemichemi za maji kutoka mlima Rungwe zinamwaga maji kwenye ziwa Nyasa.

### 1.2.2 Hali ya Hewa

Ni nchi ya kitropiki, yenye mvua nyingi kwa mwaka mm2000-3000 kutegemeana hali ya majira. Hali ya joto 22-30°c.

### 1.2.3 Utamaduni

Utamaduni ni mambo yote yanayomhusu binadamu na mazingira yake. Ni mambo yote yanayohusu elimu katika jadi, namna watu wa jamii fulani wanavyoishi. Utamaduni ni amali za jamii ikiwa ni pamoja na lugha yao, mila na dasturi, mtindo wa maisha, imani na sanaajadiya. Utamaduni hujitokeza kwa maumbo tafautitafauti, hujitokeza kama; fasihi simulizi; ngoma, nyimbo; sherehe, misiba na matambiko, Mbiti (1956). Utamaduni katika lugha yao kwa namna wanavyoitumia kuwasiliana masuala ya kwao, kuamkiana kwao, kusaidiana kwao mambo ya raha na karaha. Kwa mfano, katika raha hupeana pongezi kwa matendo kama wanawake husalimia kwa kuchuchuma na kupiga makofi (ukukoma amanja), hutoa vitu kwa moyo wa ukunjufu na kwa karaha hufanya hivyo hivyo. Uhalisiya ulionekana pale watafitiwa walipojumuika na uongozi wa ofisi ya kata ya Rufingo kwenda kutoa pole kwa wafiwa kwa kutowa katoni moja ya sukari na fedha kwa matumizi mengine.

### 1.2.4 Mila

Mila ni mambo yanayofanywa sehemu kubwa ya jamii fulani yanayolingana na asiliya na utaratibu wa nyendo za jamii hiyo.

#### 1.2.5 Dasturi

Dasturi ni kawaida ya kila siku, mazoea, ada, kanuni, sharia. Kwa mfano, kwa utamaduni wanyakyusa wana namna yao ya kusalimiana kwa kutumia lugha yao. Wanawake huwasalimia wanaume kwa kupiga magoti au kwa kuchuchumaa katika kuonesha heshima na maadili waliyokuliya. Hali hiyo huendeleya hata katika masuala mengine ya kula, kuvaa.

## 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kila jambo ama kitu kina historia yake. Binadamu kama ada ana asiliya yake, bila shaka jambo na matukio yana ualisiya wake. Dhima ya nyimbo kwa mfiwa / wafiwa katika jamii zina mapisi yake kabla hatujaelezea uasiliya wake. Hapa hatuna budi kuifafanua dhana zinazojitokeza kwenye tatizo la utafiti.

### 1.3.1 Dhana ya Mfiwa / Wafiwa

Mfiwa ni neno, jina, nomino ya kawaida linalojibainisha kwa kauli ya kutendewa, kutokewa jambo la kufiwa na ndugu mtoto, mtu mzima, jamaa wakaribu ama wa mbali. Mtu / watu wenye majonzi, huzuni, maskitiko kwa kufikwa na janga la kifiwa ama kupotelewa na ndugu.

#### 1.3.1.1 Historia Mfiwa

Historia ya kufiwa kwa mwanadamu ilianza tangu Adamu wa kwanza alipofiwa na mtoto wake Abeli na kaka yake Kaini. Kadiri wanadamu walivyozidi kuongezeka ndivyo na matukio ya kufiwa yalivyozidi kuongezeka. Sababu ya kuongezeka kwa vifo ikiwa ni uchafuzi wa mazingira. Hapo ndipo nyimbo zilipobuniwa katika kumtia faraja (Biblia na Korani).

### 1.3.2 Dhanna ya Nyimbo

Nyimbo au nyimbo ni kipera cha ushairi chenye mahadhi ya sauti ya kupanda na kushuka. Maneno ya sauti ambayo yameundwa kwa lugha ya mkato, taswira na mkong'osio wa silabi. Maneno ya sauti hupangwa kwa utaratibu maalum ili kuleta mapigo ya kimuziki.

### 1.3.3 Dhanna ya Dhima

Dhima ni kazi, umuhimu, manufaa ya kitu, jambo, au suala fulani juu ya mtu, binadamu, kama vile kuelimisha, au kuburudisha.

### 1.3.4 Chimbuko la Nyimbo kwa Wafiwa

Chimbuko ni chanzo, asili. Hivyo chanzo cha nyimbo kwa wafiwa ni matukio ya kifo, majanga, kuwepo kwa misiba, iliyotokea katika jamii. Majanga hayo yaweza kuwa yamesababishwa na uasiliya ama kusababishwa na binadamu wenyewe. Majanga ya asiliya yaweza kuwa ni mafuriko katika kusabisha watu kufa, kimbunga na magonjwa. Majanga yasiyo ya asiliya ni kama vifo vinavyotokana na vita, ama kuuwa kutokana na sababu fulani au bila ya sababu.

Ushairi ni utanzu wa fasihi simulizi. Balisdya (1989) anasema, "ushairi ni fungu linalojumlisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalum. Mapigo ya kimuziki, kupangwa kwa muwala wa urari …. Mulokozi (1989) anasema, "ushairi katika fasihi simulizi hupambanuliwa na lugha ya kawaida kwa namna unavyopanga na kutumia lugha na mbinu za kimuktadha.

Fasihi ni sanaa itumiayo lugha katika kuelezea maisha mema na mabaya ya binadamu utamaduni, mila na dasturi zilizomo katika jamii kutokana na jiografia yao, mazingira na wakati husika. Sanaa ni ufundi na ujumi autumiao binadamu katika kutoa hisi, kero fikra, mawazo kwa jamii ikiwa ni pamoja na kuelezea na kuhifadhi amali zao asiliya ya sanaa jadiya.

Wamitila (2010) anasema, " Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa namna maalum inayoathiri, na kupitisha ujumbe Fulani unaomhusu binadamu au wenye maana Fulani na inahusishwa na utungo au matini inayotambiliwa."

Mulokozi (1996) anasema, "fasihi ni sanaa ya lugha yenye ubunifu inayojaribu kusawiri vipengele vya maisha, mahusiano na hisia za watu katika muktadha Fulani."

Hivyo nyimbo kwa wafiwa zina historia ndefu kama binadamu alivyo na historia ndefu. Binadamu ana fasihi yake inayomwongoza toka kale. Asili ya fasihi ni simulizi zilizojaa tajiriba nyingi na ndefu. Fasihi hiyo imeweza kuelezea matukio, mazingira, utamaduni, mila na desturi kulingana na muktadha na wakati kama vile asemavyo Sengo (2009) kuwa kila fasihi ina kwao, jiografia na mapisi yake. Hii ina maana kwamba kila mtu kwa kabila lake, jamii, taifa lake yampasa kufahamu na kuthamini fasihi yake.

Mulokozi (1996) na Wamitila (2012) wanasema nyimbo zina sifa zifuatazo: wimbo au nyimbo husimulia kisa, kamili, huimbwa na kuchezwa mbele ya hadhira

na hadhira hushirikishwa kwa namna ya kuimba na kucheza ama kusikiliza kulingana na muktadha wa tukio.

Mc Alister (2002) anaiainisha nyimbo, kama vile nyimbo za harusi, bembezi, mbolezi wawe na kimai, nyimbo za siasa, mapenzi, kazi na nyizo. Nyimbo hizo huainishwa kutokana na uwasilishaji, kufuatana na muktadha wa tukio la utendaji. Kwa mfano, nyimbo kwa wafiwa huimbwa kwenye msiba, majanga kwa minajili ya kufariji, kuliwaza, aidha nyimbo za matambiko huimbwa kuhusiana na janga linahusu jamii hiyo. Hivyo nyimbo huwa na fani na maudhui kulingana na tukio mbali na hayo ndani ya nyimbo hizo kunakuwa na dhima kulingana na jamii yenyewe.

Jackobs (1976) anasema, “ nyimbo huwa na muundo wa beti moja, mbili na zaidi. Hujitokeza katika masimulizi ya hadithi kwa lengo la kunogesha. Nyimbo zinaweza kuwa nadhamira ya masimulizi ya kuhuzunisha au kufurahisha, kuchekesha kama vile kwenye tukio la msiba.

Semzaba (1997) anasema, “fasihi simulizi zimetokana na nadharia ya masimulizi na nadharia ya mwigo (wigo)” Miviga ambayo ilisaidia kuleta uwiano ufaao kati ya binadamu na dunia iliyomzunguka, kuwepo kwa Mungu. Binadamu aliweza kufanya ibada ya tambiko katika kupambana na matatizo yaliyomkabili. Ibada ya tambiko hazikufanyika bila ya kuhusisha nyimbo katika fasihi, ambazo wakati mwingine ziliambatana na ala za sauti kama vile kofi, ngoma, njuga au ala yoyote iliyotoa sauti. Pia walitumia mavazi maalum, maleba na mapiku kuka milisha

itikadi zao. Wanyakyusa kwa kutumia sanaa katika ngoma, nyimbo wametumia kwenye sherehe na misiba.

Nadharia ya fasihi ya simulizi ilihusisha utambaji wa hadithi. Hadithi hazikuwa na mvuto bila ya nyimbo na hadhira. Nadharia ya mwigo ya Aristotle, inasema fasihi simulizi imetokana na mwigo. Mwigo ni uundaji mpya wa kile kitu kilichopo kukifanya bora zaidi. Hii ina maana kuwa fasihi simulizi inakuwa kuendelea kubadilika kama vitu vingine vilivyo hai. Mmiliki wa fasihi ni binadamu anayekuwa na kubadilika kulingana na mazingira, muktadha wa tukio na wakati kufuatana na jiografia yake (mazingira).

Fasihi simulizi katika nyimbo kwa wafiwa, hutumia lugha ya kisanaa, yenye mguso, mvuto, mnato, picha, taswira, ishara, mafumbo na yenye lugha ya tamathali za semi. Wakati mwingine badala ya mfiwa au wafiwa kusikitika, anaweza kushiriki kuimba na kucheza akasahau shida kwa muda kutokana na jinsi wasanii, waimbaji wanavyojituma kuimba na kucheza kwa lengo la kumfariji, kama ni kufiliwa yeye si wa kwanza wala si wa mwisho. Ni katika usuli wa tatizo ndipo tumeibua dhima ya nyimbo kwa wafiwa ndipo tunajihoji, kujiuliza; je! Nyimbo kwa wafiwa zina mhusu nani? Zina umuhimu gani? Kwa sababu zipi? Bila shaka zina umuhimu wake katika jamii.

## 1.4 Tatizo la Utafiti

Tatizo la utafiti limeibuliwa katika jamii ambayo ina mapisi, muktadha wa tukio na wakati. Hii ina maana tatizo hilo limo katika jamii ndogo ni sawa na tatizo lililo

katika jamii nyingine kama taifa ama bara lolote lile. Watu wengi kutozingatia dhima ya nyimbo kwa wafiwa kumesababisha kukosekana maadili mema katika jamii (Sengo, 2009).

Katika jamii nyingi mijini na vijijini imeonekana kupuuza, kudharau nyimbo asiliya kutoka kwa wasanii hata kuwaimbia wafiwa. Badala yake watu wameona nyimbo zisizo na uzima kuwa ndiyo bora. Wanajamii hao tumeshuhudiya kwenye nyimbo mbalimbali wakitumiya vinyonyi (CD na Flash) na zamani waliita sahani za santuri walizoziweka kwenye santuri (gramfoni) zao na leo vinyoji vinawekwa kwenye radio na televisheni ama luninga na kuruhusu kuimba nyimbo kwenye sherehe za harusi, jando au unyago, ubatizo au upadrisho, kusimikwa kwa viongozi, kufiwa, matambiko, mahafari.

Utamaduni na mila na dasturi ulidumisha utu wa mtu, ukwao, uafrika. Miaka ya sasa imeonekana kukimbilia ugeni, wanausema usasa. Bado jamii nyingi tangu watoto hadi watu wazima hawazingatii maudhui na dhamira zake hasa katika kuona ubora wa nyimbo hizo katika umuhimu au dhima zake. Wanaangalia umbo la nje tu. Yaani fani katika utendaji wa nyimbo hizo.

Katika mazingira hayo ya mjini na vijijini ndiko kuliko tupelekea kuchunguza dhima ya nyimbo kwa wafiwa katika jamii ya wanyakyusa mkoa wa mbeya, Rungwe. Lengo la utafiti ni kuona kama kuna uzingativu wa dhima ya nyimbo hizo kwa wanajamii asiliya, ambayo ni sawa na jamii nyingine ya Tanzania na mahala pengi hapo.

## 1.5 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya nyimbo kwa wafiwa katika jamii ya Wanyakyusa mkoa wa Mbeya, wilaya ya Rungwe.

## 1.6 Madhumuni Mahususi

i) Kubainisha dhima za nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya.

ii) Kuchambua dhamira katika nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya.

iii) Kuelezea uhalisia wa dhima za nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa kwa jamii ya leo.

## 1.7 Maswali ya Utafiti

i) Nyimbo za msiba zina dhima gani kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya?

ii) Nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa zinawasilisha dhamira zipi?

iii) Dhima za nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa zina uhalisia gani kwa jamii ya leo?

## 1.8 Umuhimu wa Utafiti

Kukamilika kwa utafiti katika fasihi simulizi na katika nadhariya ya Kiswahili ni tunu kubwa katika taswira yafasihi ya Kiswahili. Tasnifu hii inategemewa kuleta manufaa yafuatayo: kusaidia kuchambua na kutathmini dhima ya nyimbo kwa

wafiwa na wasomi wengine. Pili, kusaidia kuongeza ari kwa wasanii kuibua vipaji vya utunzi wa nyimbo katika makabila yao. Tatu, utasaidia kutia chachu kwa watafiti wengine kufanya utafiti zaidi katika makabila ya Tanzania au Afrika. Nne, kusaidia kutoa hima kwa watafiti wengine wa kazi ya fasihi simulizi, kipera cha nyimbo kuwawezesha kuzifanyia uchunguzi kazi zao huku wakizifananisha na kuzitafautisha na kazi nyingine zilizo wahi kufanyika (marejeleo). Katika kudumisha utamaduni, mila na desturi. Kutusaidia kufufuwa Utu wa mtu, Ukwao na Uafrika. Kuwaimbia wafiwa siyo suala la mtu mmoja ni suala la watu wote kumjali mwenyezi Mungu.

Tafakuri katika nyimbo kwa wafiwa, utafiti wetu umegundua kuwa zaweza kuleta upendo, amani, furaha na maendeleo toka jamii ndogo hadi kubwa. Utafiti huu ni wazi utakuwa muhimu kwa wanakijijini wa Kinyakyusa, kabila zote na watanzania wote na wote wanaothamini utu wao, mahali popote ulimwenguni.

## 1.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti wetu umejikita katika kuchunguza dhima ya nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa kwa wafiwa na kisha kueleza uhalisia wake. Tunafahamu kuwa katika nyimbo kuna vipengele vingi ambavyo vinaweza kutafitiwa lakini sisi hatuta shughulikia vipengele hivyo bali tumetazama dhima na uhalisia wa nyimbo hizo kwa jamii tu.

## 1.10 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu yetu imeundwa na sura tano. Sura ya kwanza, inahusu utangulizi kwa ujumla, ambayo imesheheni asiliya na historia ya Wanyakyusa, usuri wa tatizo la

utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahsusi ya utafiti,maswali ya utafiti,umuhimu wa uafiti,mipaka ya utafiti na mpangilio wa utafiti na hitimisho.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadhariya. Kazi tangulizi na mikabala ya kinadharia iliyotumika katika kuchunguza na kuchambulia data za utafiti. Sura ya tatu inaeleza mbinu na vifaa mbalimbali vya utafiti tulizozitumia kukusanyia data na kuchambulia data tulizozipata kutoka kwa watafitiwa.

Sura ya nne inahusu uwasilishaji, uchambuzi wa data za utafiti uliokusudiwa kutokana na pengo la utafiti. Tumebainisha uhalisiya utamaduni, mila na desturi uliokuwepo, uliopo na unavyoendelea kubadilika kama inavyoonesha kupitia nadhariya ya mtu – utu, nadhariya mabadiliko.

Sura ya tano inahusu muhtasari, matokeo ya utafiti, matatizo ya utafiti, mapendekezo na hitimishi katika nyimbo kwa wafiwa. Maoni au mapendekezo yametolewa kwa lengo la kuboresha suala zima la utafiti kwa serikali kwa wanazuoni watafiti.

# SURA YA PILI

# 2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii imeonesha na kubainisha wataalam watangulizi walivyotalii na kusemeya kuhusiana na kazi zao walizozifanyia uchunguzi. Pia, imeonesha mikabala ya kinadhariya iliyosaidia kufanyia uchunguzi, ukusanyaji wa data na kuchambua data tangulizi. Kothari (1985) anasema kuwa, kabla mtafiti hajaanza utafiti wake hana budi ajipe muda wa kutosha kutalii yale yaliyoandikwa kuhusu somo lake. Maelezo haya ya Kothari (ameshatajwa) yalituonyesha umuhimu wa kupitia kazi tangulizi katika utafiti wetu nasi tukafanya hivyo.

## 2.2 Dhima za Nyimbo katika Jamii

Nyimbo ni moja kati ya vipera vya fasihi simulizi chenye historia ndefu katika maisha ya binadamu (Mulokozi, 1996). Inaaminika kuwa nyimbo ndio utanzu wa kwanza kupata kuwepo hapa duniani kwani karibu jamii zote zina matumizi ya nyimbo katika miktadha mbalimbali. Mulokozi (ameshatajwa) anaeleza karibu katika nyanja zote za maisha ya binadamu zinaambatana na nyimbo. Kwa mfano, katika shughuli za ibada, misiba, harusi, kampeni za kisiasa, halaiki, kutawazwa kwa kiongozi na katika kipindi cha mapumziko pia kuna nyimbo. Hii ni sawa na kusema kuwa, nyimbo zinachukuwa sehemu kubwa ya maisha ya binadamu kuliko kitu kingine chochote. Kama hivyo ndivyo, nyimbo zina nafasi kubwa katika kutoa elimu na marifa mbalimbali kwa wanajamii wote.

Taban (1972) anaeleza kuwa nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi ambacho kazi yake

kubwa ni kuliwaza wanajamii kutokana na masaibu mbalimbali ya kimaisha wanayokumbana nayo kila siku. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa kuwa ni ukweli uliokuwa wazi kwamba katika maisha ya binadamu kuna misukosuko mingi ambayo wanakutana nayo kila siku na nyimbo zinatumika kama chombo cha kuwaliwaza na kuwafanya kuyaona masaibu hayo kama ni moja kati ya changamoto za maisha na kuwa tayari kukabiliana nazo. Mawazo haya yametusaidia kupeleka mbele utafiti wetu ambao unashughulikia dhima ya nyimbo za msiba kwa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya. Msiba ni tukio zito kwa wafiwa na hivyo kuwaliwaza wafiwa ni moja kati ya mambo muhimu yanayotakiwa kuzingatiwa na kila mwanajamii. Nyimbo za msiba zinachukua nafasi kubwa ya kuhakikisha kwamba wafiwa wanapata faraja katika kipindi chote cha msiba na katika utafiti wetu tumechunguza dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya.

Naye Sengo (1978) anaeleza kuwa mila na dasturi za jamii ya watu fulani hupatikana katika nyimbo za jamii hiyo. Kila jamii ina mila na dasturi zake na kila kila jamii ina nyimbo zake z matukio mbalimbali. Hii ina maana kuwa ni katika nyimbo ndipo kunahifadhiwa miiko ya jamii kuhusu maisha ya jamii husika. Wanyakyusa ni moja kati ya jamii za Tanzania ambao wana nyimbo za matukio na miktadha tofauti tofauti zikiwemo nyimbo za msiba. Katika utafiti wetu tumechunguza dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa mkoani Mbeya na kisha kubainisha uhalisia wake kwa jamii ya leo.

Mulokozi (1999) anaeleza kuwa nyimbo ni kipeara cha fasihi simulizi ambacho

kinatumika katika kusawiri migongano ya kijamii ndani ya jamii fulani. Anaendelea kueleza kuwa katika jamii kuna baadhi ya watu wanakuwa hawaridhiki na maamuzi yanayotolewa na viongozi wao kuhusu mambo kadhaa katika maisha. Wananchi hutumia fursa ya kuimba nyimbo kuelezea kutorishwa kwao na maamuzi ya aina fulani yaliyotolewa na viongozi wao. Katika nchi ya Tanzania kwa mfano, nyimbo za Bongo fleva hutumiwa na wasanii kama chombo ya kubainisha migongano iliyopo katika jamii juu ya masuala mbalimbali ya maisha yao. Utafiti huu tumeufanya kwa lengo la kubainisha dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya na kisha kuelezea uhalisia wake.

Nao Njogu na Wafula (2007) wanaeleza kuwa nyimbo ni moja kati ya vipera vya fasihi simulizi ambacho kinatumika katika kusawiri maisha halisi ya jamii. Miongozi mwa maeneo ambayo nyimbo hutumika kusawiri uhalisi wa maisha ya jamii ni katika kuelezea masuala ya umaskini, maradhi, utabaka, kuhamasiha utendaji kazi na kadhalika. Maelezo haya tunakubaliana nayo kwani ni ukweli uliokuwa bayana kwamba ni dhima ya nyimbo kusawiri maisha halisi ya jamii kwa kutumia mbinu za kisanaa. Utafiti wetu umefanywa kwa lengo la kubainisha dhima za nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya.

## 2.3 Fani katika Nyimbo

Fani ni ile ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira yake (Njogu na Chimerah, 1999). Fani katika fasihi huundwa na vipengele vya mtindo, muundo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi ambacho nacho kimeundwa kwa kutumia vipengele

hivyo vya fani. Wapo watafiti kadhaa ambao wameshughulikia kipengele cha fani katika nyimbo kwa namna mbalimbali. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa nyimbo zina matumizi makubwa ya lugha ya mafumbo na picha hasa kutokana na matumizi yake ya lugha ya mkato. Nyimbo hutumia lugha ya mkato ili kutotumia maneno mengi na hivyo kulazimika kutumia lugha ya mafumbo na picha. Lugha ya aina hii husaaidia kueleza mambo mengi kwa kutumia maneno machache. Pia, matumizi ya lugha ya aina hii husaidia katika kuifanya jamii kutafakari kwa makini kile kinachoelezwa na mtunzi kwa makini ndipo waweze kuelewa maana yake ni nini? Katika utafiti wetu tumefanikiwa kubaini matumizi ya lugha ya aina hii ndio maana tukafanikiwa kubainisha dhima za nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa kwa wafiwa.

Jilala (2008) alifanya utafiti uliokuwa na lengo la kubainisha matumizi ya sitiari katika nyimbo za Bongo fleva ambazo zinahusu UKIMWI. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa, matumizi ya sitiari katika nyimbo za Bongo fleva yanajibainisha kupitia majina mbalimbali yanayotumika kuita UKIMWI kama vile “dege,” “ngoma,” na “miwaya.” Matumizi ya lugha ya aina hii huipa jamii fursa ya kutafakari kidogo juu ya maneno haya na baadae kuelewa vizuri dhamira iliyokusudiwa na mwandishi. Katika utafiti wetu tumecfanikiwa kutambua matumizi ya lugha ya aina hii na ndipo tukaweza kubainisha dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa mkoani Mbeya.

Ramadhani (2013) alifanya utafiti uliochnguza nafasi ya mwanamke katika nyimbo za taarab ya mipasho za Mzee Yusuf Mzee na kubainisha kuwa mwanamke anasawiriwa kama kiumbe duni. Anaendelea kueleza kuwa katika nyimbo hizo

mwanamke anasawiriwa mbeya, malaya, mfitini, mnafiki, si mwaminifu na muovu. Pia, mwanamke anasawiriwa kama mchapakazi, mvumilivu na mwenye hekima. Nafasi hii ya mwanamke kama inavyojitokeza katika nyimbo za Mzee Yusufu Mzee imeweza kuibuliwa mara baada ya kufahamu vipengele vya kifani vilivyotumika katika kuwasilishia dhamira katika nyimbo hizo. Mawazo haya yalikuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti wetu kwani nasi pia tumeweza kubainisha dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa.

Naye Omari (2009) alifanya utafiti juu ya nyimbo za Bongo fleva kama fasihi pendwa. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa nyimbo za Bongo fleva huundwa mtindo wa mashairi huru ambayo huandikwa bila kuzingatia urari wa vina na mizani ingawa yapo pia mashairi yenye kufuata urari wa vina na mizani. Kwa hakika mtindo wa aina hii unatumika kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya makabila yakiwemo yale ya Wanyakyusa. Katika utafiti wetu tumechunguza dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya ambapo pia tumeshughuliia mashairi yasiyokuwa na mtindo wa vina na mizani.

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni muongozo ambao unaeleza namna jambo lilivyo au linavyotakiwa kuwa au linavyofahamika katika maisha ya kila siku (Kothari, 2008). Maisha ya kila siku ya jamii huongozwa na nadharia mbalimbali zikiwemo zinazofahamika na zimeandikwa katika vitabu na nyingine hazijaandikwa mahali popote lakini zinatumika. Kwa utafiti ni kazi ya kitaaluma sharti ingozwe na nadharia na katika utafiti huu tumetumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi.

### 2.4.1 Nadharia ya Saikiolojia Changanuzi

Hii ni nadharia inayohusu akili ya binadamu na imeasisiwa na Sigmund Freud ambaye anaeleza kuwa kila kitu ambacho binadamu anakifanya tangu anapoaamka asubuhi mpaka analala usiku ni matukio ya kisaikolojia (Wamitila, 2002). Saikolojia ya binadamu inapokuwa imetulia ndipo binadamu anaweza kufanya kazi zake vizuri na ikiwa saikolojia haijatulia ni vigumu mwanadamu kuweza kufanya kitu ambacho kitaelezwa kuwa ni cha maana. Kwa mfano, mwanadamu anapofiwa na mtu wa karibu hupata huzuni na kuifanya saikolojia yake kuwa na mawazo sana na kushindwa kufanya jambo lolote lile mpaka baada ya muda mrefu kupita.

Sigmund anaendele kueleza kuwa mwanadamu ni kiumbe ambaye anaongozwa na mambo makuu matatu katika maisha yake ya kila siku (Njogu na Wafula, 2007). Mambo hayo ni mahitaji, raha na wasiwasi. Mahitaji makuu ya binadamu ni chakula, malazi na mavazi. Ikiwa binadamu anapata mahitaji yake ya kila siku bila taabu basi saikolojia yake itatulia na anaweza kuwa na maisha ya amani na utulivu. Inapotokea kwa bahati mbaya akakosa mahitaji hayo muhimu upo uwezekanao mkubwa wa kufanya vitendo viovu na kihalifu kama wizi na dhuluma ili tu aweze kupata mahitaji yake ya kila siku. Matukio yote hayo mawili yaani lile la kuridhika baada ya kupata mahitaji na lile la kuamua kuingia katika wizi na dhuluma ni matukio ya kisaikolojia.

Jambo lingine ambalo linatawala maisha ya binadamu ni wasiwasi katika maisha. Binadamu ni kiumbe mwenye wasiwasi katika maisha yake kwa sababu anakuwa hajuwi kesho yake itakuwa vipi (Wamitila, 2002). Upo uwezekano mkubwa mtu akawa ni kiongozi katika awamu fulani ya uongozi lakini hajuwi kama atashinda

katika uchaguzi ujao. Jambo kama hili linamfanya kuwa na wasiwasi kila siku na hivyo kuifanya saikolojia yake kutotulia na kutokana na kutokuwa na uhakika na maisha yake. Suala la wasiwasi katika maisha ya binadamu hujitokeza pia pale binadamu anapokuwa hana uhakika wa maisha mara baada ya kustaafu rasmi kazi aliyokuwa akiifanya na kukosa mshahara. Hii huwafanya watu wengi kuishi kwa hofu na hata wakati mwingine wanapoteza maisha kutokana na msongo wa mawazo unaosumbua saikolojia yao.

Jambo la tatu ambalo Sigmund analieleza kuwa ni muhimu katika maisha ya binadamu ni raha na hasa raha ya kijinsia. Binadamu ni mtu ambaye saikolojia yake kwa kiasi kikubwa inapenda kuishi maisha mazuri lakini pia kupata starehe ya kingono (Njogu na Wafula, 2007). Hii imetokea mbali kwani tangu pale mtoto anapoanza kunyonya kwa mama yake mara baada ya kuzaliwa huanza kupata raha ya kijinsia. Sigmund anaeleza kuwa wakati mtoto anaponyonya kutoka kwa mama yake kwani titi la mama huwa ni kama uume na mdomo wa mtoto hua uke. Mtoto anapokuwa mkubwa hutamani kuipata raha ya kijinsia kwa haraka ili aendelee kupata raha ya kijinsia. Raha ya aina hii na nyingine kama zile za wanajamii kutamani kuwa na nyumba nzuri, gari zuri, kwenda kumpumzika katika fukwe za bahari na katika maziwa.

Msiba ni moja kati ya vitu ambavyo vinamfanya binadamu akose raha pale unaposibu. Mathalani, kufiwa na mzazi ni kitu ambacho kimaukiza sana katika maisha ya kila simu ya jamii. Nyimbo zinazoimbwa wakati wa msiba huwaliwaza wananchi na kusahau taratibu masuala ya msiba. Jamii ya Wanyamwezi kama ilivyo

kwa jamii nyingine wanazo nyimbo ambazo zinaibwa wakati wa msiba. Tumeamua kuitumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi kwa sababu ina uhusiano wa karibu na saikolojia ya wahusika au ndugu wa karibu na marehemu na pale nyimbo zinapoibwa huwa na dhima fulani. Hivyo, utafiti huu umefanywa ili kuweza kuziba pengo la maarifa kwa kubainisha dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii tumewasilisha mapitio ya kazi tangulizi ambayo yamehusu dhima ya nyimbo na fani katika nyimbo. Mapitio hayo ya kazi tangulizi yametusaidia kubainisha kuwa hakuna utafiti ambao umefanywa kwa lengo la kuchunguza dhima ya nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya. Pia, katia sura hii tumewasilisha mkabala wa kinadharia ambapo nadharia ya Saiolojia Changanuzi.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura ilitangulia tupata pengo la utafiti kutoka katika kazi tangulizi na tuliona nadhariya walizotumia kwenye kazi zao. Baada ya kupata dira kwa kutumia nadhariya zitasaidia kuangalia mbinu na zana. Katika surahii tumewasilisha na kujadili mbinu na zana za utafiti zilizotumika. Kothari (2008) amesema, mbinu za utafiti ni muhimu katika utafiti kitaalumu kwa kuwa zinafanyika kisayansi, siyo ubabaishaji. Morrison (1993) anasema, uchunguzi humwezesha mtafiti kukusanya taarifa kwenye chanzo, ndani ya mazingira ya shughuli za jamii. Nadhariya ya Uhalisiya, Ushirikiano na nadhariya zingine zilituongoza kwenye maskani.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali, sehemu ambapo utafiti ulifanyika, mtafiti alivyokusudia kama asemavyo Cresswell (2009). Eneo la utafiti lililo kusudiwa kufikiwa ni maktabani Mwanza, Dar-es-Salaam kama vile; Chuo kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Taaluma za Kiswahili. Maktaba hizo zilitumika kutupatia data za msingi, za mwanzo na za upili katika kusoma maandiko mbalimbali, Tasnifu za wataalimu, vitabu, makala na majarida kuhusiana na mada ya uchunguzi wa dhima ya nyimbo kwa wafiwa.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni ramani au mchoro au mpango ambao unabainisha bayana namna utafiti utakavyofanywa tangu wakati wa kukusanya na kuchambua data za

utafiti (Babbie, 1999). Katika utafiti huu tumeteua uchunguzi kifani kuwa ndio usanifu wa utafiti huu. Uchunguzi kifani ni mbinu ya kueteua jambo maalumu la kulishughulikia katika utafiti ili kupata data zinazotakiwa. Sisi katika utafiti huu tumeshughulikia dhima ya nyimbo za msiba kwa jamii ya Wanyamwezi wa mkoani Mbeya.

## 3.4 Aina za Data Zilizokusanywa

Utafiti huu umekusanya data za msingi na upili kama inavyowasilishwa hapa chini.

### 3.4.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile zilizo kusanywa kwa mara ya kwanza, data halisiya ambazo hazijawahi kukusanywa na mhakiki mwingine. Goods (1966) anasema, Data za msingi huwa ni ghafi na hukusanywa kwa lengo la kuziba pengo, mwanya la utafiti lililoachwa na watafiti wengine watangulizi. Kombo na Tromph (2006) wanasema, Data za msingi katika mada yetu tumekusanya katika jamii ya wanyakyusa kutoka wilaya ya Rungwe, kata ya Lufingo, kijiji cha Kalalo, Itele na Simike.

### 3.4.2 Data za Upili

Data za upili ni data, takwimu, taarifa zilizokusanywa na wachunguzi, watafiti wengine (Best na Khan, 2008). Data hizo zilipatikana katika vitabu, makala, majarida, tovuti, tasnifu, nukuu ambazo zilihusiana na utafiti huo. Katika utafiti huu tulisoma machapisho na maandiko katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

## 3.5 Uteuzi wa Watafitiwa

Uteuzi wa watafitiwa ulipatikana kwa kutumia mbinu ya uteuzi lengwa, kusudio. Uteuzi kusudio ni sehemu ndogo ya jamii iliyochaguliwa kutumika kwenye uchunguzi ili kukidhi mahitaji ya utafiti kuwakilisha sehemu kubwa. Utafiti ulitumia uteuzi lengwa wa watafitiwa. Shulman Bryanne (1988), Burges (1999) na Kothari (1990) wanaeleza kuwa uteuzi lengwa ni mbinu ya kuteua sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua kwa makusudi akitambua kuwa sampuli hiyo ndiyo itakayompatia data anazozihitaji. Kupitia mbinu hii tuliweza kuteua sampuli ya watafitiwa 20 ambao walihusisha wanaume 10 na wanawake 10 ambao wana uelewa wa nyimbo za msiba katika jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya. Tulitumia uteuzi huo kwa sababu kuwa ndiyo unaoendana na mazingira ya mada ya utafiti kuleta uhalisiya. Aidha uteuzi ulitusaidia kupata nyimbo kwa wafiwa kutoka katika taasisi za dini na watafitiwa wasiojihusisha wa taasisi hizo, wasanii na kwa wafiwa.

## 3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti huu ulikusanya data kwa kutumia mbinu ya usaili na ushiriki kama zinavyowasilishwa hapa chini.

### 3.6.1 Mbinu ya Usaili

Ni mbinu iliyokusudiwa kutumika kukusanyia data ili kukusanyia taarifa zote muhimu katika kukidhi mahitaji yote ya utafiti. Usaili ni namna ya kuliweka jambo kimaandishi au kimazungumzo kwa ajili ya kuhifadhi kwa kumbukumbu zaidi. Best na Kahn (1998) wanasema, usaili ni majibizano ya watu wawili yenye lengo maalum

la mtafiti ili kupata taarifa zenye ushahidi kamili. Usaili hukusanya taarifa kutokana na mazungumzo ya moja kwa moja kati ya mtu na mtu.

Denscombe (1998) anasema, Usaili unajumuisha utambuzi na ufahamu kuhusu jambo linalosailiwa, lililo muhimu.Usaili unaruhusu kubadilisha swali kufuatana na wakati na mazingira.Kwa msingi huo watafiti waliweza kuwa huru kubadilisha maswali kufuatana na muktadha katika kupata dhanna iliyokusudiwa.

Keya na wenzake (1989) wanasema, Usaili nimwelekeo binafsi wakati wa usaili unaosababishwa na hali ainayo msaili, pengine kwa sababu ya tabaka, jinsia, na umri alionao. Hivyo, maswali ya usaili yaweza kuwa yameandikwa au la. Katika utafiti wetu tutatumia maswali huru na maswali ili kupata data kutoka kwa watafiwa. Mbinu hii ilitumika katika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa 20 walioteuliwa katika utafiti huu. Hawa ni waimbaji maarufu wa nyimbo za misiba katika jamii ya Wanyakyusa.

## 3.7 Mbinu ya Ushiriki

Enon (1998) anasema, ni mbinu ya kukusanya data kwa watafitiwa, wahojiwa kwa kushirikiana nao bila kuhisi kuwa wanachunguzwa. Kahn (1993) anasema, Mbinu Shirikishi ambayo mtafiti hujionea mwenyewe na kujisikilizia vitu na mambo mbalimbali vinavyoambatana na mila na dasturi za jamii husika.

Cohen na Keith (2001) wanasema, Ushiriki unamfanya mtafiti avutiwe kukusanya data zake kutoka kwenye tukio la uhalisiya. Watafiti walijumuika na watafitiwa

waliposhirikiana kwenye matukio ya misiba. Watafiti waliambatana na uongozi wa kata walishiriki kuchangia rambirambi na kushirikiana nao kwenye mazishi katika vijiji vya Kalalo na Itete (Kabale).

## 3.8 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Mbinu iliyotumika kuchambua data za utafiti ni mbinu ya kimaelezo na kitakwimu. John (2007) anasema, uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu inayo mruhusu mtafiti kusikiliza, kuona ama kusoma kazi fasihi na kasha kueleza fani na maudhui ya kazi ya fasihi.

Katika kufikia azima ya uchambuzi na dat watafiti walisoma mapitio kwa mapana na kuchunguza dhima nyimbo kwa wafiwa kwa makini. Data hizo zilipatikana kwenye maskani wakati wa matukio ya misiba na kwa wasanii, watafitiwa na watafitiwa wasio wasanii uchunguzi kifani ulitusaidia kupata nyimbo zilizokusudiwa kwenye maskani na maktabani. Hivyo nyimbo zilihifadhiwa katika daftari la kumbukumbu baada ya kuzirekodi uchunguzi ulitolewa baada ya kutolewa tarjama kwa njia ya maelezo.

## 3.9 Hitimishi

Katika sura hii tumeelezea mbinu na zana zilizotumika kukusanyia, kuchambulia data ili kutolea matokeo ya uhalisiya katika utafiti lengwa. Tumetumia nadhariya kadhaa za Kiafrika kwa sababu ndizo zinazotufaa kwa uasiliya wetu kwa fasihi na matukio katika mandhali yetu.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumepitiya kazi tangulizi za watu mbalimbali waliofanya kazi ya utafiti juu ya dhima ya nyimbo kwa wafiwa. Data za utafiti katika sura hii zimewasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti. Malengo hayo yalikuwa matatu ambayo ni kubainisha dhima za nyimbo za msiba kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa, Kuchambua dhamira katika nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa na kuelezea uhalisia wa nyimbo za msiba za jamii ya Wanyakyusa kwa jamii ya leo. Kutokana na ukaribu wa malengo haya tumeona kuwa tuyaunganishe pamoja katika uchambuzi.

## 4.2 Dhima ya Nyimbo za Msiba

Katika sehemu hii tumewasilisha na kuchambua data za utafiti zinazohusiana na dhima za nyimbo kwa wafiwa wa jamii ya Wanyakyusa wa mkoani Mbeya kama ifuatavyo:

**Sabina Fiki Kundagasya**
*Sabina ilumbu lyangu x 4*
*Twalyeghenie twe babili x 4*
*Twasipinyile twe babili x 4*
*Fiki kundangasya Fiki kudangasya*
*Lilino fiki kundangasya*
*Fiki kundangasya x 4 Fiki kundangasya*
*Lino kuti ndi nulukodomolo*
*Lino kuti ndimulwakumwanya*
*Fiki kundangasya*
*Kangi fiki kundangasya*
*Sabina ilumbu lyangu kangi fiki kundangasya.*

*KIITIKIO*
*Sabina keta kundangasya x 4*
*Ukunile kangi kundangasya x 4*

**Tarjama**
Neno Sabina ni jina la mwanamke, hivyo msanii anasema
Sabina dada yangu
Tulioana wawili
Kwa nini unanitangaza kwa nini unanitangaza
Sasa kwa nini unanitangaza kwa nini unanitangaza
Sasa unasema ukurutu umemshika
Sasa anasema nina kikohozi
Sasa unasema ninaharisha (damu)
Sabina dada yangu tena kwa nini unanitangaza. Umekaa tena unanitangaza x 4

**Maana:**
Ndoa ni siri ya wanandoa, kuchukuliana na kuheshimiana ndiyo khekima. Kusudi la wimbo ni kutoa fundisho na onyo kwa wanajamii kuheshimu ndoa na kuepuka na kifo.

Dhamira zinazojitokeza katika wimbo huo ni kifo, ndoa, upendo, umalaya. Fani; wahusika ni wanandoa, jamii. Kuna matumizi ya lugha. Kwa mfano; kuna takiriri, urudiaji wa maneno kama twalyeghene twe babili, lino, fiki kundangasya, n.k. Dhima iliyojitokeza ni kukemeya, kuelimusha na kuburudisha.

Fasihi ni sanaa inayotumiya lugha bunilizi katika kubashiri yanayojili na yaliyomo mema na mabaya kwenye jamii ya binadamu kukemeya ama kupongeza ili kuleta msawaziko katika muktadha na wakati Fulani.Kazi ya fasihi hujengeka kwa msingi wa fani na maudhui. Nyimbo kwa wafiwa, msiba, nyimbo za kufariji hujengwa kwa fani na maudhui. Fani ni vipengele vya kisanaa katika kazi ya fasihi. Vipengele hivyo ni mazingira, muundo, mtindo, wahusika na lugha. Maudhui ni jumla ya mambo yaliyomo katika kazi ya fasihi. Mambo jumuishi ni dhamira, ujumbe, maadili, na falsafa. Hivyo watafiti walibaini kuwa nyimbo kwa wafiwa nazo bila

shaka zimesheheni dhima kemkemu kwa jamii husika. Watafiti walichunguza nyimbo zifuatazo:

*AFYILE KETINA*
*E joo ketina abinile ketina*
*Andile ukwitunatuna*
*Alinkanile Mwampulo atile akabagila ndondo*
*Eee ukete lelo afyile ikwitu tuna*
*Uligwimwene ketina*
*Gwe ketina gwalinkanile Mwampulo*
*Ukete lelo ing'ombe sikulya akabula kwa Mwampulo*
*Sikulya akabula kwa Mwampulo*
*Sikulya akabula kwa Mwampulo*

**Tajrima**
Ketina anaumwa ketina
Ameanza kujikuna kuna
Alimkataa Mwampulo alisema hafai maskini
Umwone sasa amekufa anajikunakuna
Uko peke yako ketina
Ketina ulimkataa Mwampulo ulisema maskini
Ona sasa ng'ombe zinakula matundakwa Mwampulo
Zinakula matundakwa Mwampulo
Zinakula  kwa Mwampulo.

**Maana:** Ndoa ni tabia siyo mali wala sura.

Lengo la wimbo ni kuwaonya vijana wa kiume na mabinti kupenda mali na sura na maumbo bali utu wa mtu. Msanii katuonesha dhamira ya umaskini kwa kutuchorea picha ya msichana Ketina, mrembo alivyomkataa Mwampulo kwa sababu ya umaskini. Pia  msanii katumia lugha ya picha kwa  kutumiya maneno  kama ngombe, akabula (matunda) kumaanisha mafankio na utajiri.

*SYAFWANAGHA SUNGA*
*Ndagha bakipanga – syafwanagha sunga botusyila*
*Ndagha mponile ifyela – syafwanagha sunga botukulwasya*
*Ndagha mlilile ndaghabatata – syafwanagha sungha botukusyila*

*Ndagha gwisile Mwaisa –syafwanagha sungha botukusyila*
*Ndagha Mwalwesye ndagha –syafwanagha sungha botukusyila.*

**Tarjama**
Poleni wananchi-ilidhaniwa utani tulipokuwa tunazika
Poleni mumepona chuma-ilidhaniwa utani tulipokuwa tunazika

**Maana ya wimbo:** Ni wimbo wa kufarijiana wafiwa kwa kila ndugu na jamaa anayekuja msibani baada maziko. Ni wimbo unaoturejesha kwenye maadili ya Wanyakyusa, utu, ubinadamu wao kupeana pole mwenzi wao apatwapo na janga lolote.

Dhamira ya wimbo ni kifo. Fani ni muundo wa maneno na sentensi kurudiwarudiwa. Kwa mfano; neno, ndaga na maneno yanayopokewa; syafwanaga sunga botukusyila. Pia ametumia lugha ya ufananishi; neno, Ifyela kwa maana chombo cha usafiri. Maana halisiya ya kifungu hicho kinasema poleni kwa safari.

Poleni mmelia poleni wababa-ilidhaniwa utani tulipokuwa tunazika
Poleni umekuja Mwaisa-ilidhaniwa utani tulipokuwa tunazika
Poleni kwa kumuuguza poleni-ilidhaniwa utani tulipokuwa tunazika

*LOZIMELE*
*Gwagile ukulile gwandile gusambukile Lozimele, Lozimele.*
*Pamo kuti ubukangile bukukoma ihodi*
*Lozimele bukwingila ngati mbwele buno siku kwela igali, Lozimele, gwee Lozimele.*
*Lozimele .Lozimele kusabula utunywili*
*ngati malesigha Nkyunya Lozimele.*
*Lozimele x3*
*Kangi mbilike mbandu kuti ilya tata likangele Lozimele kuti litoligwe nkwangila inyama ja nfifupa Lozimele umbili ngupele jujune, nena kugonelegha, maso Lozimele Lozimele.*
*Lozimele Lozimele nalingapapo linga usambwike gumbonieghe*
*bukangale bungumwishe kubunini Lozimele gundisyghe ngati kana akafyele Lozimele Aaa Lozimele Lozimele.*

**Tarjama**
Umeona umekuwa umeanza kuniacha Lozimele Lozimele
Labda unadhani uzee unapiga hodi Lozimele

Unaingia kama inzi ziingiavyo kwenye gari
Lozimele Lozimele
Lozimele Lozimele unachana tunywele kama ulezi wa Chunya Lozimele
Tena nimesikia kwa watu unasema libaba limezeeka limeshindwa hata nyama
Ya kwenye mifupa Lozimele
Mwili nimekupa mwenyewe niliyekukeshea macho Lozimele Lozimele
Lozimele Lozimele hata kama umenizila napo uwe unanisalimia Lozimele
Uwe unanilisha kama mtoto mchanga Lozimele Lozimele Aaa Lozimele
Nakufa kimaskini kama sina mtoto Lozimele wee Lozimele
Usije ukalaaniwa bule Lozimele wee Lozimele
Uzee baraka kwa Mungu Lozimele wee Lozimele.

**Maana:** Wimbo una maana kutoa onyo na fundisho kwa jamii kwamba unapokuwa usiwadharau wazazi wanapokuwa wazee, wahudumiwe na waangaliwe kama mtoto anavyotunzwa. Kuna takriri katika wimbo,utumizi wa alama ya mshangao.

**Dhima:** Wimbo una kazi, umuhimu kwa jamii kuburudisha, kukosoa na kuelimisha wajibu wa watoto kwa wazazi wao. Msanii katumia tamathali za usemi ya tashibiha katika kulinganisha vitu, watu kwa kutumia neno kama. Kwa mfano, anasema,….unaingia kama inzi.,….unachana nywele kama ulezi wa Chunya'.Lengo likiwa ni kukemea tabia mbaya ya uhuni.Anaelimisha jamii juu ya wajibu kwa wazazi,msanii anaposema,hata kama nimezeeka uwe unaniangalia'.

*TUMOGHELE*
*Tumonghele  tumoghele – tumoghelee*
*Tufikile mwe pakusekela*
*Tufikile mwe pabweghi mwe*

*Tumoghele tumoghele – tumoghelee*
*Umwa nitu –Tumoghelee*
*Ugwa busungu – tumoghelee*

*Tumoghele tumoghele – tumoghelee*
*Tumoghele – tumoghelee*
*Jope Ngula – tumoghelee*

*Mwe abwike - tumoghelee*
*Bakipanga – tumoghele*
*Alipabwegi,nu Malafyale*
*Nu malafyale-tumoghee*
*Alipabweghi mwe nuMalafyale mwe-tumoghee.*

**Tarjama**
Tuchezee, tuchezee-tuchezee x4
Tumefika jamani harusini jamani tuchezee
Tumefika tumchezee mtoto wetu wa kwanza
Naye Ngula jamani yuko huru na mfalme
Tumchezee, tumchezee, tumchezee x4
Yupo harusini na mfalme jamani-tumchezee
Ni harusi yake ya mwisho-tushangilie jamani
Tumchezee, tumchezee, tumchezee.

**Maana:** Wimbo unawahimiza wafiwa kumwenzi, kumkumbuka kwa tabia na matendo mema aliyokuwa nayo ndugu yao aliyewatoka kwa kuwani harusi yake ya mwisho.

**Dhima:** Dhima inayotawala ni kuliwaza wafiwa kwa kufananisha kifo kama harusi. Waombolezaji Wanasikika wakisema kwa korasi neno tumchezee.

*JOSWE NSEGHETU?*
*Bati uswe joswe nseghetu tukumagha twansusu*
*Nuswe tukanile mpaka tumalisye ubwalwa bosa.*
*Eeh bajaja tubalaghe.*

**Tarjama**
Eti sisi maskini tunywe twa mwisho
Nasisi hatutaki hadi tumlize pombe yote
Eeh jamani tuwaage Wasangu hadi tumalize pombe yote x4

**Maana:** Tuache kudharau watu wa makabira mengine.

**Dhamira**; umoja, ukabila, umaskini. Wimbo unakemeya ubaguzi;kabila,tafauti ya kimapato,umoja na ushirikiano ndiyo utu na jadi yaWanyakyusa.

**Fani:** Ufutui na takiriri ya wimbo. Utumizi wa lugha;neno nseghetu-watu maskini limetumika

Kama tashititi.

*SYAFWANAGHA SUNGA*
*Syafwanagha sunga nghimba naloli x4*
*Syafwanagha – syafwanagha sunga nghimba naloli.*
*Botukulyasya safwanagha sunga - nghimba naloli .*
*Batata/bajuba syafwanagha sunga- nghimba naloli*
*Botusyila syafwanagha sunga- nghimba naloli x4*

**Tarjama**
Ilidhaniwa Utani
*Ilidhaniwa utani-kumbe kweli x4*
*Wakati tunazika ilidhaniwa utani-kumbe kweli x 4.*

**Dhima**

Waimbaji wanatukumbusha wajibu na upendo kwa jamaa zetu kama ulivyo Uafrika.Wanatuelimisha juu ya umuhimu wa kushirikiana kwenye matukio kama ya misiba, sherehe na shughuli zingine za umma. Wanasema,…tulipokuwa tunamuuguza,…tulipokuwa tunazika.

Yote hayo ni katika kudhihirisha nadhariya ya utamaduni.

Nyimbo za ngoma ya ipenengo

Hizi ninyimbo zinazotumia maneno machache

Lakini zenye ujumbe maalum kwa jamii. Ni nyimbo inayotumia vyombo vya muziki kama ngoma kubwa na ngoma ndogo ndogo zenye mlio tafauti tafauti zenye mwondoko wataratibu wakitumia singa za wanyama.Mfano wimbo ufuatao;

Afwele jombo boikujonga Eee
Eee afwele abajombo boikujonga
Eeeh ukwilelesya akalulu
Ukaghone gwa kwa Mwampulo, ukaghone gwe mwifyusi,

Ukaghone gwe ntengamojo.

**Tarjama**
Eee alivaa viatu virefu wakati anatoroka
Kwa heri mtu wa eneo la Mwampulo
Kwa heri mtu mtanashati
Kwaheri mtu mpole.

*SILI MUMAPELELE*
*Silimumapelele kana Likongonde, silimma pelele kana Likongonde*
*Baliko bamoX2 bikulogha abinaboX2*
*Baliko bamo – baliko bamo bikubinika abinabo.X2*
*Baliko bamo X2- bikubaghogha abinaboX2*
*Baliko bamo- baliko bamo bikubaghogha abinamo X2*

**Tarjama**
Ziko kwenye malisho(mabuani )mtoto(mwana) wa Likongonde.
Wako wengine wanawaloga wenzao.
Wako wengine wanawaharibu wenzao
Wako wengine wanawauwa wennzao.

**Maana:** Ng'ombe ziko kwenye majani hakuna mazao, mavuno, ni

Wimbo una maana kwamba vifo hutokeya kwa sababu mbalimbali; uchawina ushirikina na kwa fitina.Hivyo waimbaji wanalaana kukemeya sanaajadiya isiyo na tija.Kwa kutumia kejeli na mafumbo wasanii wanasema, wapo wengine wanawaloga wenzao, wanawaharibu kwa njia za kishirikina.

Dhamira zinazojitokeza katika wimbo huo ni kifo, sanaajadiya ya uchawi na ushirikina na utamaduni.

Fani zinazojitokeza ni utumizi wa lugha ya mafumbo yenye kejeli ndani yake. Wimbo umetumia lugha ya picha ya ng'ombe na majani.

Dhima ya wimbo ni kuburudisha, kukemeya matendo yote mabaya; uchawi na mauaji ya aina Yoyote.

*ALIGWA MBOMBO*
*Tummenye twesa tumenye twesa*
*Aligwambombo tummenye twesa x2*
*Tumenye twesa*
*Tummenye twesa twesa tummenye twesa*
*Alimwifyusi twesa*
*Tummenye alijojujo tisulumenie*
*Twesa tusuluminie*
*Atutulagha fijo-tummenye twesa*

**Tarjama**
Tunamjua wote tunamjua wote alikuwa mfanyakazi hodari
Tunamjua wote.
Alikuwa mfanyakazi hodari tunamjua wote tunamjua wote
Tunamjua wote tunamjua wote alikuwa mtanashati
Tunamjua wote alikuwa mwenyewe tumehuzunika
Tunamjua wote tunamjua wote.
Alitusaidia sana tunamjua wote tunamjua wote,
Tumehuzunika tunamjua wote tunamjua wote.

**Maana:** Wimbo una maana kwamba utu wa mtu ni uwajibikaji.

**Dhamira;** Utamaduni,mila na dasturi

**Fani;** takiriri

**Dhima;** wimbo unaelimisha jamii juu ya uwajibikaji mbali na kukumbuka matendo mema Ya mtu aliyefariki.

*JOANI AMBE KAJEMBA?*
*Joani ambe kajemba twangale twangale bukyex2*
*Joani ambe kajemba twangale bukye x2*
*Ugwa kuneghela amsi, ugwa kusebela imbabu,*
*Ugwa kunjengela inyumba.*
*Joani ambe kajemba aneghele amesi*
*Joani ambe kajemba ansesemele bukye*
*Joani ambe kajemba onyapile akaseke*
*Joani ambe kajemba ambemo utufu.*

**Tarjama**
Nani anipe mwozaji mwenzangu tuongee usiku kucha x2
Nani anipe mwozaji mwenzangu tusaidiane kuchota maji x2
Nani anipe mwozaji mwenzangu tusaidiane kuchuma mboga x2
Nani anipe mwozaji mwenzangu tusaidiane unga x2

**Maana:** Wimbo una maana katika jamii kuna matukio mbalimbali kwa jamii ya Wanyakyusa wana utamaduni wa kupeana vitu. Wanyakyusa wana msemo wao wa kujaliana, "Abanyakyusa bikuja ni mbatata imbinyila". Wana maana Wanyakyusa wapotembeleana hawaendi mikono mitupu bali hubeba zawadi yoyote. Nadhariya ya Utu-Mtu, ya Kiafrika,ya kila fasihi ina Kwao.

**Dhima:** Wimbo unatudhihirishia udumishi wa utamaduni, upendo, ushirikiano

*AKAJEGHE JEGHE*
*Akajeghe jebhe - kailagho*
*Mugonile ba juba- kailagho*
*Mugonile  ba tata- kailagho*
*Mugonile  bakipanga –kailagho*
*Mugonile  mwebanangu-kailagho*
*Akajeghje jeghe– kailagho*
*Mugonile  baTukuyu Akajeghe jeghe  kailagho*
*Mugonile baNgonde*
*Mugonile mweba Safya*
*Mugonile mwe Bandati*
*Mugonile mwe ba Sango*
*MugonilemwebaHehe.*
*Tumezunguka x3 tumefika x2 tumezunguka*
*Hakujambo nyumbani, tumefika tumezunguka x2*
*Hakujambo Konde (Kyela), tumezunguka x2*
*Hakujambo kwa Mwampulo, hakujambo Ibungu*
*Tumezunguka x4*
*Korasi, Akajeghe, jeghe jeghe-kailagho x2*

**Maana:** Wimbo una maana ya kuwa Wanyakyusa wana mila na dasturi ya kujali sana matukio.

Tunawasikia wakiimba, twembele x2-tumezunguka kwenye majanga kwenye misiba katika uoasiliya yao.

**Dhima:** Dhima zake ni kurithisha, utamaduni, mila na dasturi. Kama waimbavyo, tumezungu zunguka

Kwenye miji na vijiji Kyela, kwa Mwampulo, Ibungu, n.k. Matendo hayo yanaonesha umoja na upendo kwa jamii yote.

*BATWELE INDEKO*
*Bati abandumbila  batwele indeko*
*Bati batwele indeko*
*AbankaTumba bamama batwele indeko*
*Abakwa Kyela bamama batwele indeko*
*AbaNdotela bamama batwele indeko*
*Batwele indeko bamama batwele indeko*
*Abambujinga bamama batwele indeko*
*bati batwele indeko batwele indeko*

**Tarijama**
Asante sana Bandubile
Eti wameleta chungu
Wandumbila wa mama wameleta vyungu
Eti Wandumbile wamama wameleta vyungu waKyela wamama wameleta vyungu
Watukuyu wamama wameleta vyungu
Watukuyu wamama wameleta vyungu
Wambeya wamama wameleta vyungu
Wausangu wamama wameleta vyungu
eti wameleta vyungu.

**Maana:** Wimbo una maana ya kusisitiza ushirikiano kwenye matukio mbalimbali katika jamii ya Wanyakyusa.Una maana umoja kwa makabila yote, Watanzania wote.

**Dhima:** Wimbo huimbwa kwa kutumiya mafumbo na lugha ya picha. Mf, picha ya wahusika kutoka pande mbalimbali kwa majina na vyambo vyao (Abankatumba, Ababusangu, AbakwaKyela n.k.). Husifia ujio na upendo wao na uletaji wa

rambirambi; vyakula, fedha na vitu vingine kama mikeka, blanketi au shuka. Hudumisha utamaduni, mila na dasturi. Wimbo hudumisha usher ikiano na umoja matukio yote katika jamii.

Lilino lilino mbabule banangu ukwelile igali kubuka pamo kwa Mwakaleli pamo nTukuyu pamo mMbeje syope IMBWELE sikukwela mwigali.

Kali umenye ukufwa banangu imbwele sikutwala ubonywa usibingeghe mwanangu. Iminyambala gikukongesya kunyuma ngati bwele bali nubonywa mwanangu usyaganieghe, Gwisa kufwa!

Nanumwe mwe bakangale syaki isindilila mwe amabele ngati ngwego kangi mukwijubula imibili ngati njoka, gwe ugogile abandu baNtwa kisita nongwa, akupyutigwa kwa KYALA.

Sasa sasa niwambie watoto wan,gu, umepanda gari,unakwenda pengine linalokwenda pengine kwenda Tukuyu pengine Mbeya nazo inzi zinapanda garini. Sijui unaelewa kufa, mtoto wangu, hizo inzi zinaleta ugonjwa uzifukuze motto.

Wanaume wakali wanafuata nyuma kama inzi, mtoto wangu wana ugonjwa mtoto wangu, uelewe utakufa!

Nanyi wanawake wazee za nini sindilia uliye na matiti kama mkuki, tena mnajichubua miili kama nyoka, umeuwa watu wa Mungu bila sababu,utaungua kwa Mungu.

**Maana:** Wimbo una maana kwamba katika jamii kuna mmomonyoko wa maadili mema.

**Dhima:** Msanii kwa kutumia lugha ya mafumbo na lugha ya picha anakemeya wanajamii juu ya tabia mbaya ya uhuni na umalaya.

Katile Ndola
Ndo ndo ndola –katile,ndola katile
Kajuba-katile,katata katile
Nekololo –katile
Nesele-katile

**Tarjama**
Ndo ndo ndola—ilikuwa ndola ilikuwa
Mama—ilkuwa baba ilikuwa
Mimikololo(mzubaifu)-ilkuwa
Mimisele-ilkuwa

**Maana:** Wimbo unachangamsha watu waliozubaa wanaotendewa mambo mabaya na kujilaumu baadaye.

**Dhima:** Wimbo kwa kutumia korasi na ufutuhi kufundisha kukemea ujinga aliona mtu ili kujenga uchangamfu.

*EVELINA KUNDUMBUSYA*
*Evelina, Evelina, Evelina*
*Gwagile ujuba akajapo po gwandile ukundumbusya ne kana kanenino*
*Ugwe Evelina, Evelina, Evelina*
*Ijoo ijoo eeh*
*Umwana gwa nino jope gwako, Evelina kulonda ukungoga*
*Evelina mwene amenye*
*Ugwe Evelina, Evelina, Evelina,*
*Gwagile utata afwile, po gwandile ukundumbusya ne kana kanenino.*

**Tarjama**
Evelina ni jina la mtu, jinsia ya kike.

Evelina, Evelina, Evelina
Umeona mama hayupo ndiyo umeanza kunihuzunisha mie katoto kamwenzio
Wewe Evelina, Evelina, Evelina
Kibwagizo
Ijoo! Ijoo! Ijoo! Eeh!
Mtoto wa mwenzako naye wako Evelina unataka kuniua!
Evelina Mungu anajua!
Umeona baba amefariki ndiyo umeanza kunihuzunisha mie katoto ka mwenzio.

**Maana:** Wimbo una maana ya kukosekana kwa amani kwa wanandoa.

**Dhamira:** Msanii ametumia wahusika wanandoa katika kuibusha yaliyomo katika jamii. Amemtumia Mhusika Evelina kuwa chanzo cha mgogoro wa ndoa dhidi ya mme wake, baada ya kufariki baba na mama mkwe.Mme wake anasema ,umeona baba amefariki ndiyo umeanza kunihuzunisha!Kuna kukosekana kwa upendo kwa watu wengine.Kama msanii anavyobainisha:beti la pili anasema,mtoto wa mwenzako naye wako.

**Dhima:** Dhima inayojitokeza katika wimbo huo ni kukemeya mfarakano katika ndoa na kudumisha upendo kama asemavyoo msanii,…. Umeanza kunihuzunisha. Mtoto wa mwenzako naye wako.

*UNKASI GWA MWALIMU*
*Eeh! Eeh! Eeh! – Ijaja ijalejaja*
*- bandambalike juba x 4*

*Eeh! Gwekajemba, gwekajemba – bandambalike juba*
*Ijaja lejaja – bandambalike juba x 4*
*Unkasi gwa mwalimu akamanya ukuluka indefu, amenye sitanitani*
*Unkasi gwa mwalimu akamanya ukwenga ikyindi, ukwengha ikyindu ikifube*
*Eeh! Eeh! – Ijaja lejaja*
*Gwe kalumbu unkambule ukajobe linga siku*
*Gwe kalumbu unkumbule ukajobe linga siku.*

*Eeh! Tukulila – ijaja lejaja*
*Tukulila – bandambalike juba*

**Tarjama**
Korasi:Eeh! Eeh! Eeh!Ijaja-Ijaja,Ijajaleja
Wamemlaza mama x4
Mke wa mwalimu hajui kusuka mikeka anajua kufuma vitambaa
Mke wa mwalimu hajui kusonga ugali anasonga ugali mbichi.
We dada ukamwambie ukaseme kama siku
We dada ukamwambie ukaseme kama siku
Tukulila wamemlaza mama.

**Maana:** Mwanaume analia kwa sababu mke wake hajui utamaduni wa jamii yake.

**Dhima:** Wimbo kwa kutumia korasi na takriri anaelimisha juu ya hasara ya kutozingatiya Utamaduni, mila na dasturi. Mtunzi anaikumbusha jamii umuhimu uzingativu wa nadhariya ya utamaduni.Kama kusuka mikeka na kusonga ugali kwa mwanamke mwenye maadili.

*TUKUBOJA JOMBA*
*Eeh Eeh EehUgonile, Mwakasala*
*Ugonile Sankemwa-Tuboja jomba*
*Asamisye-Tukuboja jomba*
*Tukulila-Tukuboja jomba*
*Kwa Kyala mwe Twipute-Tukuboja jomba*
*Ndaga mwisile –Tukuboja jomba*
*Tukulila ajongile situtobile-Tukuboja jomba*
*Mwasande tusyele mwe tulibapina*
*Tukuboja jombaMwe nendebule-Tukuboja jomba*

**Tarjama**
Kibwagizo:Eeh! Eeh! Eeh! Hujambo Mwakasala, hujambo Sankemwa
Tunatafuta jomba
Asamisye-tunatafuta jomba
Tunalia-tunatafuta jomba
Kwa Mungu jamani tuombe-tunatafuta jomba
Asante kwa kuja-tunatafuta jomba
Tunalia,ametutoka,ametushinda-tunatafuta jomba
Mwasandende tumebaki mayatima-
Tunatafuta jomba, jamani nifanyeje- tunatafuta jomba.

**Maana:** Wimbo unamanisha kutafuta amani, faraja kwa wafiwa.

**Dhima:**Kwa kuzingatia nadhariya ya Kiafrika;Utu ni mtu,upendo katika kufarijiana kwenye majanga yaliyomo masikani.

*TUMANYENE*
*Tumanyene tumanyene tumanyene*
*Ukete abangi bamanyene*
*Ababu Sangu tumanyene, ababu Jinga tumanyene*
*AbaIgembe tumanyene*
*Umbinile nu Mosesi –bamanyene*
*Pyagilemo nu Mbokania-bamanyene*
*Ukete abangi bamanyene*

**Tarjama**
Tumepatana x3
Uone wengine wamepatana
Wausangu tumepatana, Wabujinga tumepatana, Waighembe tumepatana
Uone wengine tumepatana x3
Mbinile na Musa wamepatana, Pyagilemo na Mbokania wamepatana
Uone wengine wamepatana x3

**Maana:** Maana yake umoja ni nguvu.

**Dhamira:** Umoja, upendo.

Fani; wimbo na ufutuhi.Waimbaji kwa kutumia fani ya ufutuhi huwaimbia wafiwa nao hutakasika mioyo yao.Kutakasika ,kusuzika hukamilika kwa matendo yao kwakupeana vitu na kusaidiana katika misiba, sherehe; harusi,ubatizo, n.k.

Dhima; kuburudisha na kuelimisha kwa kusisitiza umoja katika masuala mbalimbali, kusaidiana kwenye matukio kama misiba, harusi n.k.

*TWENDENI GALILAYA*
*Twendeni Galilaya tukamtafute Bwana x2*
*Bwana wa mabwana amejaa mabwana x2*

*Wimbo huimbiwa wafiwa kwa jamii ya Wanyakyusa na waumini wa Kikiristo wa wamadhehe*
*Yote.Watafiti walishuhudia hilo waliposhiriki kwenye msiba walipokuwa masikani Kalalo na Itete.*

**Dhima:** Dhima yake ni kufariji wafiwa ukimaanisha kwamba kuna matumaini baada ya kufa kuna kufufuka. Tulio hai na wafiwa wote tutawaona ndugu na wapendwa wetu. Pia walishuhudia kuwa nyimbo nyingi ziliathiriwa na dini za Kikiristo kutoka kwenye vitabu nyimbo zilizotafsiwa kwa lugha ya Kinyakyusa(Konde na Mwamba). Kama nyimbo zifuatazo:

*Ngukupala gwe Kyala gwangu.*
*Papo une umbakisye ikisa.*
*Ngukupala Kyala gwangu*
*Papo umbokile mbufwe bwa bwila*
*Nali mungisi ngakumenye,*
*Bope ubuponelo bwali na bumo.*
*3. Lelo ngusuma gwe tata,*
*Uje nannie,usindikilege.*
*Ulutufyo na lumo tata,*
*Ulwa kukutufya bununu.*
*Gwe na papo nje mundu umbibi,*
*Ngwisa pope,usukege tata.*
*Lelo nje gwako bwilabwila,*
*Nise ngupalege bwila kumwanya.*

**Tarjama**
Nakusifu we Mungu wangu
Kwa kuwa umenionea huruma.
Naksifu we Mungu wangu.
Kwa kuwa umeniokoa mauti ya daima
2.Nilikuwa gizani sikukujua
Nao wokovu ulikuwa haumo.
3.Hata hivyo nakuomba we baba.
Uwe na mimi,unisindikize.
4.Kukusifu hakumo baba.
Namna ya kukusifu vizuri.
5.We hata niwe mtu mbaya.
Nakuja napo, unifue baba.
6.Hata niwe wako kila mara.
Nije nikusifu kila mara mbinguni.

Maana ya wimbo ni kumtukuza Mungu kwa uweza wake wote juu ya binadamu.

Hivyo uweza wa mwenyezi Mungu ukatika uhai na kifo chake.

Dhima: Wimbo unafariji, kutumainisha juu ya Mungu.

*NASOBILE ALIKUMWANYA*
*Nasobile x2 alikumwanya*
*Alikugu-alikumwanya*
*Tulonde londe nyumba-alikumwanya*
*Alikugu-alikumwanya*
*Tulondelonde mosa mungaja*
*Alikugu-alikumwanya alipo papa*
*Tulondelonde mfyamba*
*Alikugu –alikumwanya alipo papa*
*Tulondelonde mosa mmisi*
*Alikuguu-alikumwanyax2*

**Tarjama**
Nasobile ni jina la mtu
Nasobile yuko mbinguni
Yuko wapi- yuko mbinguni,
Tutafute tafute nyumbani-yuko mbinguni
Yuko wapi-yuko mbinguni.
Tutafute tafute pote migombani
Yuko wapi-yuko mbinguni.
Tutafute tafute pote milimani
Yuko wapi-yuko mbinguni-Yuko wapi yupo hapahapa.
Tutafute tafute,yuko wapi-yuko wapi- yupo hapahapa
Yuko wapi yuko mbinguni tena yupo hapahapa.
Maana:mtu aliyefariki roho yake ipo mbinguni na duniani.
Dhima:wimbo unafariji na kutumainisha kwa kutumia wigizaji huku waimbaji
Wakifanya tendo la kumtafuta aliyefariki.

*INJILI NO. 122*
*UMECHOKA, UMESHUSHWA MOYO?*
*Umechoka, umeshushwa moyo?*
*Mwambie Yesu, mwambie Yesu,*
*Una huzuni, huna furaha*
*Mwambie Yesu sasa*
  *Mwambie Yesu, mwambie Yesu,*
  *Amejulika sasa;*
  *Hayuko rafiki kama Yesu,*
  *Mwambie Yesu sasa*
*Unalia juu ya haja zako?*

*Mwambie Yesu, mwambie Yesu,*
*Mbona wazificha dhambi zako?*
*Mwambie Yesu sasa*
*Waogopa? Usihuzunike*
*Mwambie Yesu, mwambie Yesu,*
*Una hofu kwa mambo ya mbele?*
*Mwambie Yesu sasa*
*Waogopa wawazapo kifo?*
*Mwambie Yesu, mwambie Yesu,*
*Wautamani ufalme wake?*
*Mwambie Yesu sasa*

*AKIFA YESU NIKIFA NAYE NO. 47*
*Akifa Yesu nikifa naye*
*Uzima upya huishi naye;*
*Humtazama mpaka aje*
*Nyakati zote ni wake yeye*
  *Nyakati zote nimo pendoni*
  *Nyakatika zote uzimani,*
*Humtazama hata atokee,*
*Nyakati zote mimi ni wake*
*Vita sipigi visivyo haki,*
*Na q*

*NGUPASYA UMBILI GWANGU*
*Ngupasya umbili gwangu umbili gwangu*
*Ugu ambelile untwa (ugwa kumwanya)*
*Bo bikumbika une mula Mwipumba*
*Kali ngajeghe nani mula Mwipumbu*
*Basangalufu aba abagholofu*
*Bisakuja na Jesu ungwa kumwanya*
*Ngupasya ukwaganila na bamanyani*
*Abatwimbaga twesa inyimbo sya ntwa*
*Bule  mmanyani gwangu kubomba fiki*
*Buleke ubugeghe buku malika x 2*

**Tarjama**
Naogopa mwili wangu mwili wangu
Alioniumba Mungu wa mbinguni
Watakaponiweka mimi mle kaburini
Heri yao watakatifu watakuwa na Yesu wa mbinguni
2.Naogopa kukutana na marafiki
Tuliokuwa tunaimba nyimbo za Mungu
Namna gani rafiki yangu unafanya nini
Yaache maua yanaisha x2

**Maana:** Maana ya wimbo ni hofu na woga wa binadamu katika maisha.

**Dhima:** Wimbo unatutahadharisha juu ya maisha ya binadamu. Pamoja na Kuelezeya uhalisiya wa asiliya binadamu.

***BANKAKYUSA MULINIKALATA***
*Banyakyusa mulinikalata*
*Undule undule gwe lumuki*
*Keta abanghi bitendekisye*
*Bajuba mulinikalata x 2*
*Undule gwe lumuli*
*Keta abangi bitendekisye*
*Batata mulinikalata x 2*
*Undule gwe lumuli*
*Keta abangi bitendekisye*

**Tarjama**
Wanyakyusa mna barua
Unisaidie we nuru
Ona wengine wamejiandaa x2
Wamama mna barua
Unisaidie we Nuru
Ona wengine wamejiandaa x2
Wababa mna barua
Unisaidie we Nuru
Ona wengine wamejiandaa x2

**Maana:** Wimbo una maana binadamu umejitayarisha kifo kitakapokuja ama Mungu atakapoja Kukuchuwa kwenda kwenye makao mapya?

**Dhima:** Wimbo kwa kutumiya lugha ya picha unatoa tahadhali kumweka binadamu katika maadili yanayotaika katika jamii na kwa mwenyezi MUNGU. Nadhariya ya Kiafrika, Uhalisiya wa Utu ni Mtu inatudhirishia hayo kwa jamii ya Wanyakyusa na kwa  Watanzania na kwa Watu wote.

*NGWEME NE NKUSI*
*Une ngweme nenkusi nenkusi abalumiana batigi ngweme*
*Bati ngweme ne nkasi nenkusi unkasi gwangu ngwankumbula ngwankumbula*
*Nkasi gwangu abana batile kwema abalumiana ukuti batigi Kwema*
*Indumbula syangu sikumbaba sikumbaba!*
*Ukuti batii nkwema nenkusi*
*Batile kwema!! Unkasi gwake alintwele kukipatala*
*Indumbula bosipandene utata jula afyile kunongwa ja kusita kusyagania.x4*
*Kunyuma jake umwanake alinkwisa alinkuti abalumiana abanine po bandogile*
*Ukuti akafyege boulo!*
*Balimo abandu nkisu muno ababikufya kisita kusyagania linga*
*Bikuti aka leka gwe aka kalibe pope batikusyagania*
*Balinilyojo bikufya kunongwa ja amasyu amapepe x4*

**Tarjama**
Kusema jitawaze (kwema) mtu mzima, wanasema jitawaze!!
Mke wake nitamwambia, nitamwambia, mke wangu watoto wamesema nijitawaze
Vijana kuniambia nijitawaze moyo wangu unaniuma unaniuma sana
Kusema nijitawaze!! mke wake alimpeleka hospitali,moyo ulipompanda
Baba yule alifariki kwa sababu ya kujua lugha.x3
Nyuma yake mtoto alikuja kusema vijana wenzangu ndiyo walio mloga
Kuwa baba yangu afariki hivyo!
Wamo watu humu wanakufa bila kujua, unaposema hiki siyo hiki hapana wanakasirika kwa kutokujua, wanapatwa na ugonjwa moyo, wanakufa hata kwa neno dogo x4

**Maana:** Wimbo una maana kuwa watu wengi hufa kwa sababu hasira, kutokujua jambo au neno lililo semwana mtu/watu mwingine. Kwa mfano, kutokujua lughaya Kinyakyusa, Kiswahili, Kisukuma, Kinguu, ama Kihiya.

**Dhima:** Kuelimisha ni dhima mojawapo katika nyimbo kwa wafiwa si kwa jamii yaWanyakyusa tu bali kwa wale wote wenye makwao, Usanguni, Ugogoni,na Usukumani.

Msanii wa wimbo katumiya lugha ya mafumbo katika kuelezeya dhamira ya kifo.mfano, anposema, wamo watu humu wanaokufa kwa kutokujua lugha,

kunakosababishwa ujinga. Kutokujua kwaweza kusababisha; utengano, vita visivyo vya msingi.

***UBUFWE KAMOLE***
*Mwe anisenendebule bongufwa*
*Akamole kikufyima bwilabwila*
*Ubwina butikwisula siku*
*Mwebanyafyale namwe bakisu*
*Tukakaghe  akanyamana ako*
*Bunu kikumala abandu*
*Twipute kwa KYALA atupoke.*

***Tarjama***
Jamani nitaendaje wakati nakufa
Kicheche kinanifukuza kila mara
Shimo lake halijai kwa nini
Wafalme nanyi wananchi
Tukafukuze kamnyama hako
Tumwombe MUNGU atatuokoe.
Ona kanavyomaliza watu.

**Maana:** Kifo kinanifukuza.

**Dhima:** Msani ametumia lugha ya picha na ya mafumbo katika kutoa tahadhali ya kifo. Pia amekemea masuala ya uchawi na ushirikina kwa watu wanaowauwa wenzao. Anasisitiza kuzingatia afya. Tumwombe Mungu atuokoe na janga la kifo kinachotokana na magonjwa na matukio mbalimbali. Aidha msanii katumia lugha ya picha naya tamathali za semi.

***Kwa mfano;***

Neno; Akamole-mnyama kicheche anayekamata kuku. Akamole-kifo
Shimo-kuzimu
Kuna tamathali za semi; akamole kikufyima bwilabwila-kitenzi kikufyima kina maana kufukuza kama kiumbe hai.

***ABANDAMBA ILYOJO***
*Abandamba Abandamba Abandamba ilyojo*
*Eee, Eee, Eee-Abandamba ilyojo*
*Ooo, Ooo, Ooo! Abandamba ilyojo.*
*Tarjama*
*Abandamba maana yake watu wa sehemu fulani, eneo fulani au watu wa kabila fulani.*
*Ilyojo-hasira*

**Maana:** Wimbo una maana kuwa watu wa eneo au kabila fulani wana hasira. Hivyo dhima yake ni kufariji na kuelimusha jamii isiwe na hasira. Hasira husababisha kifo, kugombana na kupigana bule,bila sababu ya msingi. Hasira husababisha wana ndugu kutengana hata kuuwana.

***MWANGELE NA MWE MUBOMBILE***
*Aaa! Aaa! mwangele na mwe mubombile*
*Mwangele na mwe mubombile na mwe mubombile*
*Mulimba amaboko mbakete abana, mbakete abana*
*Mwangele na mwe mubombile Eee!*
*Mbakete abana mwe mubombile.x4*

**Tarjama**
Eee!
Hajambo nanyi mliofanyakazi, hamjambo nanyimliofanyakazi,
Mliofanyakazi mnipe mikono niwaone watoto
Hamjambo nanyi mliofanyakazi, hamjambo nanyi mliofanyakazi
Eee! Niwaone watoto, nanyi mliofanyakazi x4

**Maana:** Wimbo una maana ya pongezi, shukrani kwa shughuli walizofanya. Pia wimbo una maana ya kuagana ili kwenda kuwaona watoto baada ya kukaa msibani.

**Dhima:** Wafiwa huimbiana wimbo huo ili kupeana kheri katika janga, msiba. Dhima yake ni kufariji na kudumisha undugu na upendo. Kwa mfano, anasema,”mwangele

namwe mubombile mulimba amaboko mbakete abana”(mnipe mikono niwaone watoto).

***ANDASONI MAMA***
*Andasoni Andasoni mama!*
*Usyeghe usyeghe usyeghe-Andasoni mama x3*
*Andasoni, Andasoni mama*
*Usyeghe, usyeghe, usyeghe-Andasoni mama x3*
*Usyeghe ulwa mmajolo-Andasoni mama*
*Andasoni Andasoni mama.x4*

**Tarjama**
Andasoni ni jina la mtu.
Andasoni Andasoni mama!
Usage, usage, usage-Andasoni mama!
Andasoni mama! X3
Usage kama jana-Andasoni mama!
Andasoni, Andasoni mama x4

**Maana:** Maana ya wimbo ni kukilaani kifo. Kwa masikitiko, kwa huzuni wafiwa wanasema,”usage, kama jana”. Haina maana kuwa kifo kiendelee kutokea.

**Dhima:** Wimbo unaonesha umuhimu, kazi katika kukemeya na kulaani watu wanasababisha kifo kwa Njiya uchawi na ushirikina. Wasanii wametumia lugha ya mafumbo na kejeli. Pia wametumia Tamathali za semi ya tashibiha inayotumia viungani vya, kama. Anaposema,”Andasoni usage kama jana”.

***LYABUNA***
*Aaa! Aaa! Aaa! Lyabuna lyabuna!*
*Lyabuna kwa Kyela, lyabuna kwa Mwampulo,*
*Lyabuna Mumbeje x4*

**Tarjama**
Aaa! Aaa! Aaa! Limeunguruma, limeunguruma
Limeunguruma Kyela, limeunguruma sehemu ya Mwampulo (Tukuyu).
Limeunguruma Mbeya x4

**Maana:** Maana yake kifo kimefanishwa na chombo cha usafiri kama gari linalounguruma lianzapo kutembea. Wasafiri, wafiwa hawana budi kujiandaa. Hivyo kifo ni kama njiya ya kila mtu.

**Dhima:** Wimbo unatoa taarifa ya kujiandaa juu ya kifo binadamu hajui atakufa lini. Kifo kipo Kwa Mbwiga, kesho kwa Mwanashali, Bujonde.

## 4.3 Mjadala wa Data za Utafiti

Dhima ya nyimbo kwa wafiwa katika jamii ya Wanyakyusa wilaya ya Rungwe, Kata ya Rufingo:

### 4.3.1 Kufariji Wafiwa

Karibu nyimbo nyingi za misiba zinafanya kazi ya kufariji, kuliwaza wafiwa kama tulivyo zibainisha huko nyuma. Haijalishi nyimbo hizo zinaimbwa kwa kilugha ya jamii husika ama kwa lugha gani,za dini au zisizo za dini.

### 4.3.2 Kurithisha Utamaduni, Mila na Dasturi

Nyimbo hizo huweza kutumika katika kurithisha mambo mazuri yaliyomo kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa mfano, wimbo wa mke wa mwalimu hajui kusuka mikeka…..anajua kufuma tu.Katika jamii ya Kinyakyusa mwanamke hana budi kujua kusuka mikeka kwa ajili ya kulalia, kukalia, kuzikia n.k.

### 4.3.3 Kuhimiza Umoja

Kazi nyingine ya nyimbo hizo ni kuhimiza umoja na upendo. Kwa mfano, wimbo unaosema," ukete abangi bamanyene" yaani ona wengine wanapendana. Upendo

kwa Wanyakyusa unadhihirika kwa matendo zaidi, hupeleka vitu kwenye misiba kama, mahindi na maharage, kuni, maji n.k.

### 4.3.4 Kuonya Jamii

Nyimbo zinaionya jamii ili kuirudisha kwenye maadili mema. Kwa mfano, wimbo unaosema, Wamo wengine wanawaloga wenzao. Sabina mbona unanitangaza.

### 4.3.5 Kusifia Uwajibikaji

Nyimbo pia hutumika kukumbuka ndugu waliokufa kwa matendo mema. Mfano, Wimbo wa tumjua alikuwa anafanya kazi.

## 4.4 Fani katika Nyimbo kwa Wafiwa

Fani ni njia anazozitumia msani, mtunzi katika kuwasilisha maudhui kwa hadhira husika. Fani ni umbo la nje linalobeba maudhui. Fani hujumuisha; muundo, wahusika, lugha na matumizi ya lugha na mtindo. Nyimbo kwa wafiwa katika kazi ya kuleta ufani wake kwenye tukio, watunzi na waimbaji hutumia mtindo na mbinu mbalimbali kama vile korasi na ufutuhi kwa hadhira yake. Aidha msanii hutumia lugha yenye mnato na mkato. Sanaa katika nyimbo hutumia taashira;kitu husimama kwa niaba ya kingine. Tashibiha; matumizi ya lugha katika kulinganisha kitu kimoja kwa sura, sifa au tabia kwa kutumia kiingizi cha ni. Kuna utumizi wa lugha ya picha, taswira. n.k.

## 4.5 Hitimishi

Katika sura hii tumewasilisha matendo, tabia na mambo yale tuliyoshuhudi kwenye maskani ya utafiti. Tumeona kuna mabadiliko katika fani hii kwenye uwathilino wa

lugha ya Kiswahili na lugha ya Kinyakyusa. Hivyo tumeweza kukusanya, kuchambua, kutathimini na kuwasilisha matokeo mjadala wa data za utafiti wetu.

# SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura ya nne tumeona uchunguzi wa vidhibitishi halisiya juu ya dhima za nyimbo kwa wafiwa katika jamii ya Wanyakyusa. Tumetathimini na kupata matokeo yanayoonesha dhima mbalimbali; kufariji, kuelimusha, kukemeya, kuburudisha, kulithisha utamaduni, mila na dasturi n.k. Sura hii imetoa hitimishi, muhtasari wa matokeo ya utafiti, na mwisho tumetoa maoni au mapendekezo katika kuboresha tafiti nyingine.

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti ni Kuchunguza Dhima ya Nyimbo kwa Wafiwa katika jamii ya Wanyakyusa wilaya ya Rungwe, mkoa wa Mbeya.Uteuzi wa watafitiwa ulipatikana katika kata ya Rufingo kwenye vijiji vine; Kalalo, Itete (Kabale), Simike na Kagwina.

Utafiti umeweza kutoa matokeo ya madhumuni mahsusi katika kuweza kukusanya nyimbo kwa wafiwa na tumeweza kubaini dhima mbalimbali zilizomo katika nyimbo hizo; kufariji, kuburudisha, kukemeya, kuonya, kupongeza, kulaani matendo na tabia mbaya, kurithisha utamaduni, mila na dasturi n.k. kwa wanajamii.

Aidha utafiti umeweza kuonesha mchango wa vipengele vya fani katika kufanikisha ufanisi wa nyimbo kwa wafiwa. Fani katika utumizi wa lugha ya tamathali za semi,

mafumbo, picha au taswira, n.k. Nyimbo kwa wafiwa zinakabiliwa na matatizo kama fani zingine. Tatizo kubwa ni matumizi wa nadhariya ya mabadiliko, ukuaji wa sayansi na teknolojia katika ulimwengu wetu. Nadhariya ya Wigo imeuwa uasiliya, Nyimbo za jadi nyingi zimepotea. Nyimbo za taasisi za dini ndizo zimeshika kasi kwenye mazishi na kwa wafiwa.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Baada ya kutembelea maskani tuliweza kukusanya nyimbo kwa wafiwa, kujionea matukio na matendo ya uhalisiya. Tuliweza kuchunguza na kubainisha dhima zilizomo katika nyimbo hizo kuwa kuna kuwalilia wafiwa kwa kujifanya, matendo ya utu yamepungua tulibaini kuwa nyimbo nyingi za jadi zimefuwawa kwa sababu ya kukosa aqili si za darasani wala vidato au visomo vya juu. Kudharau, kupuuza ya asili ni kujiua mwenye,hivyo dhambi. Nyimbo zinazotawala vilioni ni zadini za vitabuni na nyimbo za kwaya.

## 5.4 Mapendekezo

Tasnifu hii imelenga kurudisha moyo kwa wale walivunjika na kukata tamaa juu ya utamaduni, mila na dasturi za jadi yao. Kusudi letu ni kufufuwa utamaduni, mila na dasturi za asiliya zilizofuwawa kwa hila ya wakoloni na wajumbe, mawakili wao waeneza dini ya kigeni, mawakili hawa walidai kuwa utamaduni, mila na dasturi za nyanya, babu, baba zetu asiliya ni za kishenzi, kikatili.

Ikizingatiwa kuwa kila Taifa, nchi, jamii inayo asiliya yake. Naijulikane kuwa kila Fasihi ina Kwao. Wanyakyusa wa nyimbo za mbolezi, nyimbo kwa wafiwa.

Kutokana na pengo la utafiti tumeona kuna maadili mema katika nyimbo kwa wafiwa. Nyimbo nyingi kwa wafiwa pamoja na kuwafariji, kuwaliwaza na kuwaondolea huzunihuwa zina wasoka wanajamii kwa mambo mengi yasiyositahiki katika jamii husika kuwa elezeya na kuwasifiya mema waliyoyatenda. Nyimbo zinaelimisha masuala mbalimbali kama vile afya na uchumi na masuala ya utawala.

Tukio la kifo ni tukio lisilo badilika wala kukwepeka kwa kila binadamu aliyeumbwa na mwenyezi Mungu. Kama ndivyo binadamu hana budi kukabiliana na change moto hii, njia pekee ni kujenga umoja, ushirikiano, jumuiko katika kuwaimbia wafiwa kwa minajili ya kuwafariji na kusaidia kuondoa msongo wa mawazo juu ya wapendwa wao. Hii ikiwa ni kuwaelezeya wasifu wa wafu wao.

Mbali na wageni na mawakili wao pia kuna ugonjwa wa kufisha kabisa; utandawazi, (utandawizi), wigo usiotija uletao dharau juu ya nafasi asiliya kwa madai ya kwenda na wakati. Khali hii ni sawa na mtu anajiangalia kwenye kioo na kukataa sura, umbo lake mwenyewe na kutaka kujibadilisha kwa kujipaka rangi anazo fikiri kuwa ndiyo usasa.

Kuelimisha jamii ndogo, kama kabila hata jamii kubwa; taifa (nchi) na kujithamini na kujiamini. Kujenga uafrika wetu kwa upya na uasili wetu, utaifa wetu na ujamii wetu wa kabila zetu za asiliya. Hii ni katika kujijenga katika utu wetu na maadili mema ya kwetu "utu wa mtu ni mtu, kujijua mwenyewe ni unyama" kupuuzwa na kudharauliwa kwa nyimbo za jadi kwa wafiwa na kukumbatia utandawazi ni kupoteya kama siyo kufa kwa utamaduni, mila na desturi za wanyakyusa na kwa

makabila mengine. Yatupata kufundisha wanajamii ngazi zote kupenda na kuenzi utamaduni wetu makanisani, miskitini na mashuleni kwa lugha zetu asiliya na kwa lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Sambamba na hilo yatupata kuandikwa vitabu na kuhifadhiwa maktabani toka ngazi ya kata hadi taifa.

Fasihi simulizi kama somo lifundishwe shuleni kwa vitendo kwa lugha asiliya ya wahusika, wataalamu wa sanaa jadiya wafundisha asiliya. Wanafunzi wafundishwe kupenda asiliya yao, utamaduni wao na wakuheshimu mila na desturi zao na kuwafanya wawe wabunifu.

Serikali kwa kutumia vyombo vyake vya taalimu, wizara ya elimu na ufundi kuongezwa katika mitaala ya masomo. Ikiwa ni pamoja na nyimbo kwa wafiwa. Hivyo wanajamii watambue kuwa nysimbo kwa wafiwa hazina dhima moja bali kuna dhima nyingine ndani yake.

## 5.5 Hitimishi

Katika sura hii tumezungumzia matokeo ya utafiti wetu juu ya uchungu wa dhima za nyimbo kwa wafiwa katika jamii ya Wanyakyusa, wilaya ya Rungwe, mkoa wa Mbeya.Tumeona kuwa hazina dhima tafauti na dhima za nyimbo zingine; kufariji, kupongeza, kuelimisha, kuonya, kukuza lugha, kudumisha utamaduni, mila na dasturi. Pamoja na umuhimu wake kwa jamii bado kuna changa la macho, ufu wa aqili kwa udanganyifu wa moyo.

Misiba ni ya binadamu yeyote, maadili mema kuzingati Utu wa Mtu, Uhalisiya wa Kiafrika, Ukwetu siyo Ukwao.Mapendekezo yametolewa kwa kuzingatia kuwa ujumii wa utamaduni, mila na dasturi ndiyo msingi wa maendeleo yetu.

## MAREJELEO

Abdallah, A. (1973). "Ushairiwa Kiswahili na Uhusishwe Usiuliwe" Katika zindiko, Dar-es-Salaam: Chama cha Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Tanzania.

Aguwu, V. K. (1988). Music in the Funeral Traditions of the Akpafu of southern Ghana, *Journal of the Society f*or *Ethnomusicology Vol. 32 No 1*

Balisidya, M. L. (1979). "Utafiti, Mbinu na ukusanyaji wa Fasihi Simulizina Haiba yake, Lughayetu, Dar es Salaam: TPH.

Best, J. W. & Kahn, J. V. (2004). *Research in Education,* New Delhi: Prentice hall of India.

Buliba, A. (2015). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti,* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd,

Cohen. L. L. M. & Keitle. M. (2001). *Research Methodology Education*, London: Routlege farmer.

Denscombe, M. (1998). *The Good Research for Small Social Reseach Projects,* Buckihari: Open University Press.

Enon, C. J. (1995). *Education, Research, Statistics and Measurement*, Kampala, Makerere Uniersity Press.

Enon, J. C. (1998). *Educational Research Statistics and Measurements*. Kampala: Makerere University Press.

Finnegan. R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford: University Press.

Hoopes, J. (1979). *Oral History: An introducation for Students*, Carolina: Chapel Hill.

Finnegan, R. (1976). *Oral Literature in Africa*, Nairobi: Oxford University Press.

Khamisi, S. A. (1983). Nafasi ya fasihi simulizi katika jamii ya Tanzania, *Mulika* Na 15, Dar-es-Salaam: Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili.

Khatibu, S. M. (1982). *Pambazuko la Afrika*, Arusha, East Africa publication. Ltd. Arusha Tanzania

Sengo, T. S.Y. M. na Kiango, S. (2012). *Hisiya zetu*, Dar-es-Salaam: TUKI.

Kothari, C. R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (1993). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: India, Wiley Eastern Ltd.

Lukanga, M. (1988). "The Role of Song amagost Zigua, B.A. Dissertation", University of Dar-es-Salaam: Dar es Salaam Tanzania.

Lyndon, H. (Editor) (1966). *Poems from Kenya.* Milwaukee: The University of Wisconsin Press.

Mbogo, E. (2008). *Ngoma ya Ng'wana Malundi*. Dar es Salaam: Nyambali Nyangwine Publishers.

Meyer, T. (1993). *Wakonde, Maisha, Mila na Desturi za Wanyakyusa*, Mbeya: Motheco Publications.

Mgogo, (2012). Tasnifu juu ya Nyimbo za Misiba Zina Dhima Nyingi Jamii ya Wanyiha, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania.

Mlama, P. (1973). "Music in Tanzania traditional theatre, the kaguru as a Case study" M. A. thesis, University of Dar-es-salaam, Tanzania.

Mnyampala, M. N. (1971). *Historia, Mila na desturiza wagogo,* Dar-es-Salaam: East African Literature Bureau.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: East African Publishers Ltd.

Mulokozi, M, M (1996). Fasihi ya Kiswahili, Dar-es-salaam Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwakasaka. S. (1978). *Oral Literature of the Banyakyusa*, Nairobi: General Printers Ltd.

Ndulute, C. (1972). The Place of Songs in Hele Oral Literature M. A, Dissertation, Dar-es-salaam: University of Dar-es-Salaam, Tanzania.

Ndungo, C. W & (1991). *Misingi ya nadharia ya fasihi ya Kiswahili*, Nairobi, Mwai, University of Nairobi

Ndungo, M. (1993*). Nadharia ya fasihi simulizi*, Nairobi: University of Nairobi Press.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*, *Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nketia, J. H. (1962). *The Music of Ghana*, Accra: Longmans.

Ntilo, S. J. (1972). *Desturi za Wachagga*; Nairobi General Printers Darlington Road. 114 African Literature Bureau.

Nyagati, J. B. (1990). *Habariza Wamwera*, Ndanda: Ndanda Mission Press.

Olpewho, I. (1992). *Africa Oral Literature. Backgrounds, Character and Continuity.* Bloomington: Indiana University Press.

Omari, M. (2015). *Tatizi za Nyimbo za Wamatumbi*, Dar es Salaam: Karijamer Print Technology.

Samara, E. M. A. (1992). “The Social Function of Luo Burial and General Songs, B, A, Dissertation (Oral Literature),” Dar es Salaam: University of Dar-es-Salaam, Tanzania.

Sangu, A. S. (2000). “The Contents and Forms of the Fipa Funeral Songs, B.A Dissertation”, Dar-es-Salaam: University of Dar-es-Salaam, Tanzania.

TUKI, (2003). *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*, 3 FASIHI, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Tanzania.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi*, *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho namba 1: Usaili**

**Utangulizi**

Mimi ni mwanafunzi Kibungu Thimoth wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ninayesoma shahada ya Uzamili katika Kiswahili. Naomba mshiriki katika utafiti wangu ambao kwa sasa nipo katika hatua ya kukusanya data ili kukamilisha utafiti masomo yangu. Naombeni sana msaada wenu.

**Utambulisho**

Jina………………………………………….

Umri………………………………………..


Elimu……………………………………….

**Maswali**


1. Naomba unitajie nyimbo za msiba zinazoimbwa katika jamii ya Wanyakyusa.
2. Kwa nini nyimbo hizo huimbwa katika msiba?
3. Nyimbo hizo huwa zinabeba dhamira gani?
4. Imeshawahi kutokea katika msiba kukosekana nyimbo?
5. Naomba nieleze jambo lolote muhimu kuhusu nyimbo ambalo mimi sikuliuliza.

**Asanteni sana kwa msaada wenu**

**Kiambatanishi Na.  II: Kuonyesha Wilaya ya Rungwe na Mipaka Yake**



**Kiambatanishi Na.  II: Kuonyesha Wilaya ya Rungwe na Kata Zake**




*Source:* United Republic of Tanzania (1957, 1960, 2004c)

**FIGURE 1:** Map of Rungwe District showing location and division of wards.

**Kiambatanishi Na.  I: Mtafiti na Mshauri Wake Mwabuka (2016)**



**Kiambatanishi Na. II: Mratibu Elimu Kata Sadiki Abrahamu Mwasomola Amkaribisha Mtafiti, Ofisi ya Kata ya Rufingo (2016)**



**Kiambatanishi Na. IV: Watafitiwa Wakiwa Kwenye Eneo lao la Kuchezea Ngoma ya Jadi (Ing'oma) kijiji cha Itete**



**Kiambatanishi Na. V: Mtafiti Akiwashukuru Watafitiwa kwa Ushiriki Wao (2016)**

